epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumamosi Machi 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581624
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**Biteko** aionya wizara kuhusu miradi ya maji

UKURASA 2

**Kesi** Mbunge Gekul madai unyanyasaji yaanza



UKURASA 4

**Waziri** aagiza kufutwa leseni 2,648 mfu za madini

UKURASA 5




**GREALISH KUPIGWA BEI MAN CITY**

UKURASA 22

# Mbowe aibua mazito mishahara wabunge

• **Adai** sasa wanalipwa mil. 18/ kwa mwezi, wenyewe wang'aka...*Endelea ukurasa 2*



## Mbaroni madai kuua mke kumzika ndani, kulawiti watoto

UKURASA 4



Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa

## TPA, DP World zawatega wafanyakazi

UKURASA 2

**MICHEZO** **BOSI WA WAAMUZI AUNGA MKONO VAR** UK.24

**KATUNI** UK.6



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Murilo, akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma ya usafiri mtandaoni ijulikanayo kama SUKA, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mbowe aibua mazito mishahara wabunge

**Na Waandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ameibua hoja mpya kwa madai kwamba wabunge wamejiongezea mishahara kutoka Sh. milioni 13 hadi Sh. milioni 18 kwa mwezi.

Amesema wabunge wamejiongezea mishahara hiyo wakati wananchi wanataabika na upandaji wa bei za bidhaa na hali ngumu ya maisha.

Akizungumza juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika mji wa Babati, mkoani Manyara, Mbowe alisema: "Mpaka tunatoka bungeni (mwaka 2020), mimi na (Godbless) Lema tulikuwa wabunge tunajua tunalipwa mshahara wa Sh. milioni 13 kwa mwezi. "Hiyo ni bila ya posho ya siku ya kikao. Posho ya kikao kimoja kwa siku ilikuwa Sh. 220,000," alisema.

Kwa mujibu wa Mbowe, wabunge walijiongezea mishahara mwaka jana wakati wananchi wakiendelea kupata shida ya mfumuko wa bei.

Alisema uchumi wa nchi ulivyo kwa sasa unakuwa wa watu wachache na kwamba kuna watu wanaishi peponi na kuna wengine kama wanaishi jehanamu. "Wananchi asilimia 70 wanaishi maisha ya umaskini na tofauti ya kipato imekuwa kubwa mno. Gharama za chakula, mafuta na tozo vinapanda. Maisha yanazidi kuwa magumu na sisi tusiposema nani atasema?" alihoji Mbowe.

Wakati huohuo, Mbowe alitangaza kuanza kwa maandamano kila makao makuu ya mkoa ya Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Mbowe, CHADEMA imekita kambi Babati, Manyara, kwa ajili ya kuandaa maandamano hayo ya amani, yanayotarajiwa kuanza Aprili 22, mwaka huu hadi Aprili 30.

"Tutaandamana kwa amani, tunataka wananchi ambao wanaona gharama za maisha ni kubwa tuingie barabarani ili tudai kupungua kwa mfumuko wa bei," alisema Mbowe.

**KAULI ZA WABUNGE**

Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Kasheku 'Musukuma' alipoulizwa kuhusiana na madai hayo, alisema: "Hilo nadhani ungempigia Spika. Kwanza mimi sijawahi kuona mshahara, sijawahi hata kufungua akaunti kwa ajili ya mshahara." Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, majibu yake hayakutofautiana na mwenzake ambaye alisema,:"Maslahi ya wabunge ungemuuliza Spika ndiye angekueleza. "Mbunge ana taasisi yake ambayo ndiyo yenye majibu. Hupaswi kumuuliza mbunge individual (binafsi). Unavyoniuliza ni kama mwandishi ambaye hujui taratibu tangu lini Mbunge akazungumzia maslahi yake?" alihoji

Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alipoulizwa kuhusu madai hayo, alisema, "Mimi sijui. Niliulizwa nikasema silijui kwa hiyo siwezi kuwa na neno la kusema kuhusu hilo."

# Biteko aonya wizara kuhusu miradi ya maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, ametoa maagizo 10 na kuonya Wizara ya Maji isimkwamishe Rais Samia Suluhu Hassan katika utekelezaji wa miradi ya maji ili wananchi wapate huduma kama alivyoahidi.

Dk. Biteko pia amewahimiza watanzania kuendelea kutoa maoni katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 kuhusu suala la maji.

"Ninaomba tusimkwamishe Rais Samia anatoa fedha zitumikee ipasavyo katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji, simamieni utendaji kazi wenu ili wananchi wapate majisafi na salama," alisema hayo jana katika kilele cha Wiki ya maji jana jijini hapa.

Maagizo mengine aliyotoa ni taasisi za bodi za mabonde kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kudhibiti uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji.

Aliwataka kushirikiana na sekta binafsi kutekeleza miradi ya maendeleo, wajenge utaratibu wa kuhifadhi takwimu za maji na ukarabati wa miundombinu, waongeze kasi ya utendaji kazi.

Biteko alisema wizara inapaswa kushirikiana ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira ambao utachafua vyanzo vya maji na kuzuia upatikanaji wa maji na kuhadharisha kuwa wasipodhibiti upotevu wa maji, kila siku viwango vya maji kwa matumizi ya mtu mmoja vitaendelea kupungua.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema wizara yake itaendelea kutekeleza maagizo waliopewa na serikali ili kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama mijini na vijijini.

Aweso alisema mradi wa maji wa Same umefikia asilimia 86 katika utekelezaji na kumwakikishia Naibu Waziri Mkuu kuwa, utakamilika kwa wakati ili wananchi waweze kupata maji safi na salama.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Seleman Jaffo, aliwapongeza Wizara ya Maji, huku akiwataka kuendeleza uchapakazi ili wananchi wapate maji.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalla Ulega, alisema bila maji hakuna mifugo wala uvuvi, hivyo wizara hizo zitaendelea kushirikiana katika utendaji kazi wake.

Katika hatua nyingine, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) wamesaini mkataba wa Sh. bilioni 87.6 na kampuni ya China Railway company ili kuboresha huduma ya maji safi na usafi wa mazingira katika eneo la Mtumba.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
18.03.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **25.03.2024 hadi 31.03.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha magari matupu wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga** kuelekea **Bandari ya Dar Es Salaam,** gari hizo zenye namba za usajili **NRB97300 / NRB54202 DS00TG GP / NRB53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.5** |
| **Upana** | - | **Mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Mzenga** hadi **Bandari ya Dar Es Salaam** kupitia **Barabara ya Morogoro, Barabara ya Mandela** magari yatasafiri muda wa Mchana ***( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

117890802

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


# TPA, DP World zawatega wafanyakazi wa bandari

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA Ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imetoa tangazo kwa watumishi wa Bandari ya Dar es Salaam likiwataka kuchagua ama kubaki katika ajira TPA au kusitisha mikataba na kujiunga na ajira mpya katika kampuni ya DP World.

Taarifa ya TPA iliyotolewa Machi 20, mwaka huu, na Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, ilisema Oktoba 22, 2023, mamlaka hiyo iliingia mkataba na Kampuni ya DP World ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kuhusu uendeshaji wa gati namba sifuri hadi namba tatu na gati namba nne hadi namba saba za Bandari ya Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka 30.

"Kutokana na makubaliano hayo yanayohusisha usimamizi na uendeshaji wa maeneo tajwa, watumishi wa Bandari ya Dar es Salaam wanapaswa kuchagua kati ya kubaki TPA au kusitisha mkataba wa ajira kati yao na TPA au kusitisha mkataba wa ajira wa TPA na papo hapo kuajiriwa upya na kampuni ya DP World," ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, uongozi wa TPA umekamilisha mchakato wa utoaji wa elimu kwa watumishi wote walio kwenye maeneo husika. Taarifa pia ilisema mchakato wa utoaji elimu ulianza Machi 4 hadi 19, mwaka huu, kwa lengo la kuwapa watumishi wote uelewa sahihi wa mabadiliko ya uendeshaji yanayoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam.

"Pamoja na masuala mengine, elimu hii inahusisha mabadiliko ya uendeshaji wa bandari, utaratibu wa makabidhiano, utaratibu wa mtumishi kusitisha mkataba na TPA na papo hapo kuajiriwa upya na kampuni ya DP World kwa mtumishi atakayekuwa ameamua kufanya hivyo kwa hiari yake mwenyewe bila kushurutishwa. "Pia kuna stahiki ambazo zitatolewa na TPA kwa mtumishi atakayeamua kusitisha mkataba wa ajira wa TPA na kuajiriwa upya na Kampuni ya DP World,".

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kwa msingi huo, watumishi wa Bandari ya Dar es Salaam wanajulishwa kuwa makabidhiano kati ya TPA na DP World yameanza kutekelezwa kwa kuwa, mchakato wa utoaji elimu kwa watumishi umekamilika.

"Watumishi watakaoamua kuajiriwa upya na kampuni ya DP World wanatakiwa kufika na kuorodhesha taarifa zao jengo la TPA Makao Makuu ukumbi wa mikutano ghorofa ya 32 kabla au ifikapo Machi 29, mwaka huu," ilisema.

TANGAZO


Nipashe
MWANGA WA JAMII
Ushajua Jambo gani hilo kubwa Linakuja?
iPP
CARES FOR YOU
The Guardian
www.ippmedia.com



Askari polisi wakiwa wameubeba mwili wa marehemu Beatrice Haiyasi, baada ya kuufukua ndani ya nyumba aliyokuwa akiishi katika kijiji cha Kimamba A, wilayani Kilosa mkoani Morogoro jana, anayedaiwa kuuawa na mume wake Januari 1 mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni madai kuua mke kisha kumzika ndani, kulawiti watoto

**Na Beatrice Shayo**

MKAZI wa Kijiji cha Kimamba A, Kilosa mkoani Morogoro, Mohamed Omar (37), anadaiwa kumuua mke wake, Beatrice Haiyasi (32), na kumzika ndani ya nyumba waliyokuwa wakiishi.

Tukio la mauaji hayo linadaiwa kutokea Januari Mosi, mwaka huu, na baada ya hapo mwanamume huyo anadaiwa alikuwa akiwafanyia vitendo vya ukatili watoto watatu wa mama huyo kwa kuwaingilia kinyume cha maumbile.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka, akizungumza na mwandishi wa habari hiii jana, alisema Beatrice aliacha watoto watatu, wa kwanza wa kike mwenye umri wa miaka 11 na wadogo zake wawili wa kiume wa miaka tisa na minne.

Alisema mtuhumiwa huyo baada ya kufanya tukio hilo, alikuwa akiwafungia watoto ndani ya nyumba na kuwalazimisha kuingiliana wenyewe kwa wenyewe na wakikataa alikuwa anawang'oa meno kwa chuma. "Unyama mwingine aliokuwa akiwafanyia watoto hao ni kuwasugulia pilipili machoni," alisema.

Shaka alisema vyombo vya ulinzi na usalama vikiongozwa naye, vilifanya kazi ya kufukua mwili huo jana. Shaka alisema taarifa walizozipata kutoka kwa wasamaria walisikia mwanamke huyo akipigwa siku hiyo lakini hawakujua kilichoendelea mbele kwa sababu si watu wanaochangamana na jamii.

"Taarifa zaidi ndani ya familia zinasema mpaka anafariki (dunia) mtuhumiwa alimwuliza 'kwa namna nilivyokujeruhi kwa hiki kipigo nikumalize ama nikuache. Mama huyo alimjibu nimalize lakini nitunzie watoto wangu'.

"Kitu ambacho kinauma hata hawa watoto hakuweza kuwatunza zaidi ya kuwadhalilisha na kuwafanyia vitendo vya kinyama. Kwa sisi ambao tumeenda na kuona baada ya kufanya tukio hilo alichimba shimo katika chumba walichokuwa wakiishi kama mtu na mkewe na kumfukia kwenye shimo lenye urefu wa futi mbili na nusu," alisimulia.

Shaka alisema baada ya kumzika, mtuhumiwa huyo aliendelea kuishi katika chumba hicho na kuweka mafiga juu ya kaburi hilo na kupika chakula ili kuharibu ushahidi.

"Jambo la kunisikitisha kabisa baada ya kufanya mauaji haya alianzisha uhusiano na mwanamke mwingine na huyo mwanamke akaja kuishi katika chumba hicho alichokitumia kumzika mkewe," alisema.

Shaka alisema mtoto wa kwanza, mama huyo amezaa na mwanamume ambaye yuko Arusha na watoto wawili ambao ni wa kiume baba yao yuko Moshi na tayari taratibu za kuwajulisha wanafamilia zimefanyika na hatua inayofuata ni kuchukua mabaki ya mwili na kusubiri taratibu zingine.

Alisema watoto wa marehemu walipoulizwa, walieleza unyanyasaji walipitia ikiwamo kukosa huduma muhimu za elimu kutokana na kufungiwa ndani. Alisema watoto hao wamekutwa na majeraha ya kung'olewa meno ya mbele kwa kutumia nyundo.

Shaka alisema mauaji hayo yamebainika baada ya mtuhumiwa huyo kudaiwa kuuza mabati ya mwanamke wake wa sasa na kutokea ugomvi.

Alisema wakati wa ugomvi huo watoto wa marehemu wakawa wanamkanya mama huyo asigombane na baba yao kwa kuwa atauawa kama mama yao.

Alisema baada ya ugomvi huo ndipo mama huyo alipoliarifu Jeshi la Polisi kuwapo kwa mauaji hayo.

Majirani ambao hawakupenda majina yao yaandikwe gazetini walisema familia hiyo ilikuwa ngeni katika eneo hilo na ilikuwa haichangamani na jamii.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama, alisema wanamshikilia mtuhumiwa huyo kwa uchunguzi zaidi na upelelezi utakapokamilika atafikishwa mahakamani.

# Kesi ya Gekul madai unyanyasaji yaanza kusikilizwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA Kuu, Kanda ya Manyara, imeanza kusikiliza mapingamizi matatu ya upande wa utetezi katika kesi ya unyanyasaji inayomkabili Mbunge wa Babati Mjini (CCM), Pauline Gekul, iliyofunguliwa na mfanyakazi wake, Hashim Ally.

Jana, Wakili Ephraim Kisanga anayemwakilisha Gekul katika shauri hilo, aliwasilisha mapingamizi matatu ya rufani ya jinai, namba 577 ya mwaka mwaka huu.

Akiwasilisha mapingamizi hayo mbele ya Jaji Devota Kamuzola anayesikiliza kesi hiyo, Wakili Kisanga alidai kuwa pingamizi la kwanza walilo nalo ni mahakama hiyo haina mamlaka ya kisheria kusikiliza rufani iliyotolewa na mrufani, Hashim Ally.

Kwa mujibu wa Wakili Kisanga, pingamizi lao la pili ni kwa mrufani kushindwa kutafuta njia nyingine mbadala ya kisheria tofauti na rufani.

Pingamizi la tatu, alidai ni kuhusiana na notisi (ilani) iliyotumika kufungulia kesi ya msingi, ambayo ni rufani namba 577, ilikuwa haikidhi vigezo vya kisheria kuitwa notisi.

Baada ya kuwasilishwa mapingamizi hayo, Jaji Kamzola alitoa nafasi ya kujibu hoja za upande wa mrufani, anayewakilishwa na mawakili Peter Madeleka, Thadey Lister na John Masanja.

Akijibu mapingamizi hayo, Wakili Madeleka alidai kuwa hoja za mapingamizi zilizowasilishwa na wakili wa utetezi, hazina mashiko kwa sababu mahakama hiyo inayo mamlaka ya kisheria chini ya kifungu cha 359 na 361, kupokea rufani zote zinazotokana na uamuzi wa mahakama za chini.

Aidha, Wakili Madeleka alidai kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), hakuwa sehemu ya kesi, hivyo hakukuwa na sababu yoyote na mamlaka ya haki ya kuingilia kesi hiyo.

Aliendelea kudai kwamba kwa namna ambayo DPP aliingilia, hata hati ya kutokuwa na nia ya kuendelea na mashtaka, haikuingizwa mahakamani kwa njia zinazoelekezwa kisheria.

Madeleka aliendelea kudai kwamba mrufaniwa ambaye ni Pauline Gekul, Desemba 27 mwaka 2023 wakati shauri likiwa mahakamani kwa ajili ya kusikilizwa, hakuwapo mahakamani, huku sheria ikielekeza kabla kesi yoyote ya jinai haijaendelea, ni lazima mshtakiwa awapo mahakamani.

Alidai ni muktadha wa sheria, kusomewa mashtaka yake ili kukiri au kukataa chini ya kifungu cha 228 (1), cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), hivyo matakwa hayo ya kisheria yasipofuatwa, yanafanya mwenendo mzima pamoja na amri zilizotolewa kuwa batili.

Kutokana na hoja za pande zote, Jaji Kamuzola aliahirisha kesi hiyo hadi Aprili 15, mwaka huu, mahakama hiyo itakapotoa uamuzi kuhusu mapingamizi hayo.

Katika shauri la msingi, Gekul alikuwa akikabiliwa na shtaka moja la shambulio na kusababisha madhara kwa mwili chini ya kifungu cha 241 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, Marekebisho ya Mwaka 2022.

Alikuwa anadaiwa kuwa yeye na watu wengine ambao hawako katika malalamiko hayo, Novemba 11, 2023, mjini Babati mkoani Manyara, walimwita Hashim na kumweka kizuizini huku wakimtishia kwa silaha ya moto, walimvua nguo na kumshambulia kwa kumlazimisha kukalia chupa ya soda ili iingie katika njia yake ya haja kubwa.

# Waziri aagiza kufutwa leseni 2,648 za madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, ameagiza Tume ya Madini kufuta leseni 2,648 za utafutaji wa madini ambazo wamiliki wake wamehodhi maeneo bila kuzifanyia kazi.

Aidha amebainisha kuwapo maeneo mengi ya utafutaji madini nchini yaliyohodhiwa na watu wachache wakiwamo watu sita wanaomiliki ekari milioni 13.5 bila kuzifanyia kazi.

Kutokana na hali hiyo, Mavunde amemwagiza Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini kufuta leseni na maombi ya leseni hizo zikiwamo za watu hao sita waliojimilikisha maekari huku akisisitiza kuwa hajakurupuka katika uamuzi huo.

Akizungumza jijini hapa jana, Waziri Mavunde alisema kumekuwa na baadhi ya wamiliki wa leseni ambao wamekuwa hawazingatii utekelezaji wa majukumu yao umiliki wa leseni kwa mujibu wa Sheria ya Madini, Sura 123.

"Ninatoa onyo kali kwa wamiliki wa akaunti za waombaji na usimamizi wa leseni kwa njia ya mtandao ambao wameonyesha matumizi mabaya ya usimamizi wa mfumo kwa kuwasilisha maombi kwa lengo la kuhodhi maeneo bila kumalizia taratibu za uombaji waache tabia hiyo mara moja.

"Vinginevyo akaunti zao zitafungwa na ninatoa mfano, kuna watu sita wanahodhi maeneo yenye ukubwa wa ekari milioni 13, ukubwa wa maeneo hayo ni sawa na ukubwa mara nne wa mkoa wa Kilimanjaro.

"Hayafanyiwi chochote ilhali mahitaji ya maeneo ya uchimbaji ni mkubwa sana hapa nchini na hasa kwa wachimbaji wadogo ambao wamekuwa na mchango mkubwa sana katika kukuza sekta ya madini," alisema.

Mavunde alisema miongoni mwa makosa ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara ni pamoja na wamiliki wengi wa leseni kutoanza au kutoendeleza maeneo ya leseni zao na badala yake kuyahodhi, na kutolipa ada stahiki za leseni.

Pia alisema kutowasilisha nyaraka muhimu kama Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania kwenye Shughuli za Madini, Mpango wa Wajibu wa Makampuni kwa Jamii na nyaraka za taarifa za fedha kuonyesha matumizi yaliyofanyika pamoja na vielelezo vya matumizi husika.

Mavunde alisema utaratibu wa kufuta leseni zisizofanya kazi utakuwa endelevu mpaka hapo watakapopatikana watu makini kwenye sekta ya madini.

"Kundi kubwa la wachimbaji wadogo wamekuwa wakihangaika kutafuta maeneo na kundi la wawekezaji ambao wako tayari kuwekeza na hakuna maeneo

"Lakini watu wachache wameifanya sekta ya madini wanaweza kuitumia kama mgongo wa kutafuta kujiimarisha kipato kwa kuhodhi maeneo makubwa na baadaye kutafuta fursa ya kunufaika na maeneo hayo ili hali serikali inapoteza mapato kutokana na maeneo hayo hayo kushikiliwa.

"Hatuwezi kuwatumia wachimbaji wadogo kuwa chanzo cha utafiti, kwani tunawafanya watumwa katika nchi yao, tunataka katika sekta yetu tunakuwa na wawekezaji halisi, tuwe na watu ambao kwa dhati kabisa wanaweza kufanya uwekezaji ili nchi yetu isipoteze mapato.

"Ukiwa na eneo la ekari 13 ambalo halifanyiwi kazi ipasavyo si afadhali tukawapa wachimbaji wadogo wakaingiza mapato ya serikali kuliko utaratibu wa sasa," alisema.

Waziri huyo alisema kuna mikoa mingi ambayo kuna maombi ya leseni za utafutaji wa madini, lakini hazifanyiikazi na kusisitiza kuwa, wizara imeanza kusafisha mfumo wa utoaji wa leseni ili kuwapata watu halisi watakaofanya uwekezaji katika sekta ya madini.

Kadhalika, alisema katika leseni hizo kuna mtu mmoja ambaye pekee yake ana maombi ya leseni 973 ambazo zina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 23,118 lakini hafanyi kazi bali amezishikilia tu.

"Tumefika mwisho, tumeanza na utaratibu huu, tunaendelea kusafisha mpaka tuwapate watu ambao wako tayari kufanya uwekezaji na kufanya shughuli za madini,"alisema.

Hata hivyo, alisema leseni hizo zilipaswa kufutwa Novemba, mwaka jana, na kuwa kwa sasa tayari anaorodha ya leseni za Desemba na Januari, mwaka huu, ambazo ziko mbioni kufutwa pia.

"Nitazifuta kwa kuwa hatuwezi kuiweka nchi inashikilikwa na watu wachache wanahodhi maeneo makubwa ambayo hayafanyi kazi, wale wote wamiliki ambao hajazingatia sheria wajiande tunakwenda kusimamia sheria ili mwisho wa siku tuwapate wawekezaji halisi," alisisitiza.

Alisema kutokana na baadhi yao kufanya kosa la kutolipa ada stahiki za leseni, kiasi cha takribani Sh. bilioni 36 zinadaiwa kutoka kwa wamiliki na waliokuwa wamiliki wa Leseni za Utafutaji wa Madini, Leseni za Uchimbaji Mdogo wa Madini na Leseni za Uchimbaji wa Kati na Mkubwa wa Madini.

Katika uchambuzi uliofanywa na Tume ya Madini, imebainika kuwa, hadi Februari, 2024 kuna maombi 2,180 ambayo hayajalipiwa ada stahiki za maombi, huku kukiwapo na maombi 409 ya muda mrefu ambayo wamiliki wake wamelipa ada za maombi, lakini hawajawasilisha nyaraka muhimu zinazoambatana na maombi hayo.


## NOTISI/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD na AMA'Z AUCTION MART & GERERAL BROKER LTD** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya Siku Saba (kama rudio la mnada) na Siku Kumi na nne (14)kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CAPEVIEW COMPANY LIMITED | MUSSA SIMBA KALIMANZILA | RESIDENTIAL LICENCE NO TMK/MBGK/KGC7/129 | MBAGALA KUU,MTONI KIJICHI, TEMEKE MUNICIPALITY | 30/03/2024 4:OO ASUBUHI NA KUENDELEA (Marudio) | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 2 | OSCAR BONIFACE KAZIULAYA | LUCY W LYATUU | CERTIFICATE OF ACCUPANCY TITLE NO 84432 | MBAGALA KUU,TEMEKE MUNICIPALITY | 30/03/2024 7:00 MCHANA NA KUENDELEA (Marudio) | LEHALEL GROUP OF COMPANY |
| 3 | SUNRISE COMMUNICATIONS COMPANY LIMITED | CONSOLATA THOMAS MAKOBA | RESIDENTIAL LICENCE NO ILA/UKG/MRK33/14 | UKONGA,MARKAZI,ILALA MUNICIPALITY | 8/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY |
| 4 | ABDALLAH HAJI NOMBOLE | ZABIBU M MBONDE | RESIDENTIAL LICENCE NO TMK/MBGL/KNY28/157 | MBAGALA,KWA NYOKA, TEMEKE MUNICIPALITY | 9/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY |
| 5 | ROSE EMMANUEL GADAU | ROSE PHILEMON BAKENGA | SALES AGREEMENT | KIBAMBA MTAA WA MLOGANZILA,UBUNGO MUNICIPALITY | 15/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY |
| 6 | JOEL MATHEW GUMBO | JUDITH JOHNSON KILEO | RESIDENTIAL LICENCE NO ILA/KWN/YNB15/104A | KIWALANI,YOMBO ,ILALA MUNICIPALITY | 17/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY |
| 7 | DOTO P MADUKWA | LEYLA KHALIDY AHMED SHEBE | CERTIFICATE OF OCCUPANCE TITLE NO 161600 | MBANDE,KISEWE , TEMEKE MUNICIPALITY | 12/04/2024 SAA 6;00 MCHANA NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY |
| 8 | DANIEL JOSEPH MAGIGE | MERY DANIEL | SALES AGREMENT | KITUNDA,MZINGA (MAGOLE),ILALA MUNICIPALITY | 19/04/2024 SAA 3:30 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY |
| 9 | HALFAN JOHN MGAYA | HALFAN JOHN MGAYA | SALES AGREEMENT | CHAMANZI MAGENGENI, TEMEKE MUNICIPALITY | 16/4/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY |
| 10 | OMARI IDDI AMIRI | OMARI IDDI AMIRI | NYUMBA | VUDOI, MWANGA MJINI, WILAYA YA MWANGA, KILIMANJARO | 1/5/2024 SAA 4:00ASUBUI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 11 | OMARI IDDI AMIRI | OMARI IDDI AMIRI | NYUMBA | USANGI ,WILAYA YA MWANGA, KILIMANJARO | 27/4/2024 SAA 4:ASUBUI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 12 | RASULI ALLY MSOFE | RASULI ALLY MSOFE | NYUMBA | LEMBENI, WILAYA YA MWANGA, KILIMANJARO | 29/4/2024 SAA 4:ASUBUI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 13 | ESTER W.CHAKALA | ESTER W CHAKALA | NYUMBA | VUDOI, MWANGA MJINI, KILIMANJARO | 1/5/2024 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada ata lazimika kulipa malipo ya siyopungua 25% ya bei iliyo fikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hatimiliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenyenyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) niza mnunuzi mwenyewe.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| | |
|---|---|
| **LEHALEL GROUP OF COMPANY LTDP.O.Box68172**<br>**Dar es Salaam, Tanzania**<br>**Tel: 0620 848 565/ 0714 598 559**<br>**Email: lehalelglc@gmail.com** | **AMA'Z AUCTION MART & GERERAL BROKER LTD P.O. Box 62163**<br>**Dar es Salaam**<br>**Tel: 0658 100 737/ 0678 220 068**<br>**Email: amazauctionma@gmail.com** |

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ujenzi uwanja mpya Arusha utoe chachu kuwepo timu Ligi Kuu Bara

**SERIKALI** juzi kupitia kwa Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk Damas Ndumbaro ilitangaza kusaini mkataba wa ujenzi wa uwanja mpya wa kisasa jijini Arusha na mkandarasi kutoka nchini China.

Makubaliano ya Mkataba huo yanatoa fursa sasa kuanza mchakato wa ujenzi huo muhimu kuelekea katika uandaaji wa fainali za Afrika (AFCON) mwaka 2027 ambapo Tanzania kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda watakuwa wenyeji wa fainali hizo.

Kabla ya ujenzi wa uwanja huo mpya utakaoitwa Dk Samia Suluhu Hassan, Arusha walikuwa na uwanja mmoja unaomilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) wa Sheikh Amri Abeid ambao ni wa zamani na umekuwa ukitumiwa kwenye michezo mbalimbali ya soka.

Kwa hatua hii tunaipongeza Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa ujenzi huu wa uwanja mwingine mkubwa wa kisasa baada ya uwanja wa Benjamin Mkapa wa jijini Dar es Salaam uliojengwa enzi ya utawala wa Rais Jakaya Kikwete japo wazo lake lilitolewa enzi za utawala wa awamu ya tatu chini ya Rais Benjamin Mkapa.

Uwanja huu wa Arusha utakuwa alama kubwa kwa wanamichezo na wadau wa michezo ya kumkumbuka Rais Samia siku zote pale atakapokuwa ametoka madarakani, tunaipongeza sana serikali kwa maamuzi ya ujenzi wa uwanja huu.

Kwa bahati mbaya, kwa miaka ya karibuni jiji la Arusha limekosa kuwa na timu Ligi Kuu ya Tanzania Bara na kupelekea mashabiki na wapenzi wa soka kushindwa kushuhudia michezo ya Ligi Kuu katika jiji lao.

Michezo pekee ambayo wamekuwa wakiishuhudia kwenye uwanja wa Sheikh Amri Abeid ni ile ambayo timu ya mkoa mwingine inaamua kuchagua kuchezea michezo yake kwenye uwanja huo au michezo ya hatua ya mtoano au fainali ya kombe la Shirikisho, FA.

Soka la Arusha liliondoka kwenye ramani ya ratiba za Ligi Kuu tangu kuzorota kwa timu ya AFC ambayo ndio timu iliyokuwa ikishiriki Ligi Kuu kutokea jijini humo.

Kwa muda mrefu sasa Arusha inapambana kupata timu ya kushiriki Ligi Kuu na kwa sasa klabu ya Mbuni inayoshiriki ligi ya Champion inapambana kusaka nafasi ya kuwemo kwenye ligi kuu msimu ujao japo mambo yao hayawaendei sawa.

Tunaamini uwepo wa uwanja mpya ambao umetakiwa kukamilika kwa asilimia kubwa kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, kutaongeza hamasa ya soka katika jiji hilo.

Chama cha soka cha Arusha, kina kazi kubwa ya kuhakikisha uwepo wa uwanja huo kunaenda na uwepo wa angalau timu moja kwenye ligi kuu Tanzania Bara.

Uwanja huo uongeze hamasa kwa klabu za Arusha zinazoshiriki Championship na ligi daraja la kwanza kuiona fursa watakayoipata kama watafanikiwa kucheza Ligi Kuu na uwepo wa uwanja huo utakaokuwa na uwezo wa kuchukua mashabiki 30,000.


Tayari Arusha imepata uhakika wa kuwa na uwanja mpya na wa kisasa, kazi imebaki kwa Chama cha soka mkoani humo, wadau wa soka na wafanyabiashara wakubwa kuhakikisha wanakuwa na timu kwenye Ligi Kuu ili kutoa fursa ya kibiashara kwa wakazi wa jiji hilo hasa kunapokuwa na michezo ya Ligi Kuu.

Hataipendeza kuwepo na uwanja huo mkubwa lakini hakuna timu ya ligi kuu itakayoutumia uwanja huo kwenye michezo mikubwa ya Ligi Kuu inayohusisha klabu kubwa kama Simba, Yanga au Azam FC.

Arusha changamkieni fursa hii ya kuwepo kwa uwanja mpya na wa kisasa pale utakapokamilika, hakuna haja ya kuona timu kutoka nje ya jiji hilo ndio wanaokuja kuutumia uwanja huo na kuwaletea klabu za Simba na Yanga.

Kikubwa ni kupambana, kushikamana na kushirkiana kuhakikisha jiji la Arusha linakuwa na timu inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara na kufanya jiji kuchangamka kwenye nyanja ya michezo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## Tuliwapokea wanafunzi wa Sudan, kwa nini isiwe Al Hilal kwenye Ligi?

Na Adam Fungamwango

**NAKUMBUKA** Juni mwaka jana, Tanzania ilipokea kiasi cha wanafunzi 150 kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, Khartoum nchini Sudan.

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ilithibitisha kupokea wanafunzi hao ambao waliomba kuendelea na masomo yao ya mwaka wa mwisho kwa vitendo katika hospitali jijini Dar es Salaam.

Mapigano ambayo yanaendelea nchini Sudan yanaendelea kusababisha maafa kwa maelfu ya raia wa taifa hilo kuikimbia nchi yao ambayo ndiyo yalisababisha wanafunzi hao kuwa miongoni mwa waathirika wa machafuko hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya taifa ya Muhimbili, Profesa Mohammed Janabi akawahakikishia kuwa wamekuja sehemu sahihi na watafanya kila linalowezekana kuhakikisha wanamaliza masomo yao kwa salama na amani.

Ujio wa wanafunzi hao ulileta utani mkubwa kwenye mitandao ya kijamii kama ilivyo kawaida ya Watanzania.

Watanzania ni miongoni mwa watumiaji wakubwa wa mitandao ya kijamii katika Bara la Afrika, ambapo wakati mwingine huitumia kwa kupeleka ujumbe kwa njia ya mzaha na utani kama ilivyo kawaida, na si kwa wagomvi, bali hupenda mijadala na utani.

Hivi karibuni, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), lilitangaza kuipokea timu ya mpira wa miguu ya Al Hilal kutoka huko huko Sudan na kwa sababu hizo hizo.

TFF ilitangaza kuingiza timu hiyo kwenye ratiba ya michezo ya Ligi Kuu msimu ujao japo matokeo yao hayataathiri msimamo wa ligi hiyo.

Baada ya kutangazwa hivyo na TFF, cha kushangaza baadhi ya mashabiki wa soka wameonekana kupinga mpango huo, wakidai ni kuidhalilisha Ligi ya Tanzania.

Hata sasa unashangaa, kwa nini sababu za kuwapokea wanafunzi ziwe sawa, lakini za timu ya mpira wa miguu ziwe si sawa?

Binafsi naona kinachofanyika ni kile kile, kuifanya timu hiyo kwanza wachezaji wake kukaa sehemu salama lakini pia kushiriki shughuli za kimichezo.

Timu hiyo imeomba kucheza ligi Tanzania ili wachezaji wake wawe fiti pale watakapokuwa wanakwenda kucheza mechi za kimataifa kwa sababu Sudan kwa sasa hakuna ligi na haijulikani vita itaisha lini.

Ndiyo maana si timu hiyo tu, hata waamuzi nao wamechukuliwa kwa ajili ya kuchezesha ligi msimu ujao.

Nia ni ile ile tu kama ya wale wanafunzi.

Binafsi naipongeza TFF, Wallace Karia mwenyewe kama Rais, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambapo naamini kuwa kwa pamoja wamebariki hilo.

Ni kama wale wanafunzi, ambapo naamini Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zilihusika katika mchakato mzima wa kuwapokea.

Ninachoshauri wakati wa kwenda kutengeneza kanuni za kuiruhusu Al Hilal kucheza Ligi kuu Tanzania Bara msimu ujao kusiwe na kona kona, ziongezwe timu ili kuwa 18, pamoja na yenyewe, lakini ipewe pointi tatu ikishinda na timu ikiifunga ipewe pointi tatu na hili lifanyike hadi mwisho wa msimu.

Baada ya hapo ikiwa ya kwanza, basi bingwa atakuwa yule aliyeshika nafasi ya pili, na ikishika moja kati ya nafasi nne za juu, timu ya tano ndiyo ihesabiwe moja kati ya timu nne za juu.

Binafsi siungi mkono eti ikishinda isipewe pointi au timu ikiifunga isipate pointi, hili si sawa.

Ili kuipa nguvu Ligi ni lazima kuwe na ushindani, ikiwa ya kwanza ipewe pesa zake za mshindi wa kwanza, lakini isiwe bingwa wa nchi.

# Halmashauri zabanwa fedha mikopo ardhi

**Na Munir Shemweta,** SHINYANGA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, ameziagiza halmashauri zote nchini zilizokopeshwa fedha kwa ajili ya programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi (KKK), kutafuta vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya kuzirejesha ili halmashauri zingine zinufaike.

Pinda aliagiza hayo juzi mkoani hapa wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilipotembelea na kukagua utekelezaji mradi wa Uimarishaji Usalama wa Milki za Ardhi nchini (LTIP) kata ya Ibadakuli, Manispaa ya Shinyanga.

Alisema hayo baada ya PAC kutaka kujua hatua zinazochukuliwa na wizara baada ya kuelezwa kuwa Manispaa ya Shinyanga ni moja ya halmashauri zilizopewa fedha hizo kwa kukopeshwa Sh. bilioni 1.055 na kushindwa kuzirejesha kwa mujibu wa makubaliano.

"Halmashauri zote nchini zitafute vyanzo vingine kwa sababu hili jambo limeulizwa mara kadhaa na wizara tumeeleza mkakati tunaoenda nao," alisema.

Kwa mujibu wa Pinda, wizara kwa sasa haiangalii tena malengo ya mradi katika kupata fedha na badala yake inaenda mbali zaidi ili halmashauri zitumie vyanzo vingine kulipa deni na wakati huo halmashauri zikitumia vyanzo vingine kupata fedha.

Aliitaja Halmashauri ya Chalinze mkoani Pwani kuwa itakuwa ya mfamo kwa kuwa tayari imeonyesha nia ya kulipa Sh. bilioni 2.5 inazodaiwa kupitia vyanzo vingine.

Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, amesema kamati yake italishuggulilia suala hilo la kususua urejeshaji mikopo ya programu ya KKK na kuona namna ya kulishauri Bunge.

alisema msingi mkubwa wa serikali kutenga fedha za mkopo kwa ajili ya mradi wa KKK ni kutaka programu hiyo kuwa endelevu na mwisho wananchi waweze kupatiwa hati milki za ardhi.

"Tunataman kila kipande cha ardhi yetu ipangwe, ipimwe na kumilikishwa na ikianyika hivyo ndiyo tutaona thamani ya ardhi yetu" alisema Mhe, Hasunga.

kuhusu mradi wa LTIP uliotembelewa na PAC, Pinda alisema mradi huo katika Manispaa ya Shinyanga ulianza Oktoba, mwaka jana, kwa lengo la kurasimisha vipande vya ardhi 20,000 ifikapo Juni 30, mwaka huu.

Amesema hadi sasa vipande vya ardhi 21,850 vimetambuliwa, 7,175 vimepangwa na viwanja 1,315 vimepimwa na kwa ujumla kazi hiyo imetekelezwa kwa asilimia 51 na kazi ikiendelea.

LTIP ilibuniwa ili kutatua changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikiikabili sekta ya ardhi kwa muda mrefu.

Changamoto hizo ni pamoja na mabadiliko ya teknolojia katika utekelezaji wa kazi za sekta na utoaji huduma za ardhi, kukosekana kwa miundombinu wezeshi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika ofisi za ardhi pamoja na kasi ndogo ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi.



Naibu Spika wa Bunge, ambaye pia ni Mbunge wa Ilala, Mussa Azzan 'Zungu' (katikati) akiwa na Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughle (kushoto) na Meneja Mauzo wa kampuni ya Gesi ya Orxy , Shaban Fundi (wa pili kushoto), wakimkabidhi mtungi wa gesi ya kupikia Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Zone namba 7 katika Soko la Samaki la Kimataifa la Magogoni, Saidi Mpinji wakati wa makabidhiano ya mitungi ya gesi ya Orxy 700 kwa mamalishe na babalishe sokoni hapo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TIC kuvutia uwekezaji wa Dola bilioni tano

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania TIC), kimeweka lengo la kusajili miradi 1,000, kuvutia mitaji ya kigeni yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni tano na kuvutia mitaji ya ndani ya Dola bilioni 3.5.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan madarakani.

Kwa miaka mitatu iliyopita, alisema kituo kimefanikiwa kusajili miradi 1,188 yenye thamani ya Sh. trilioni 38.3 na kuifanya Tanzania kuongoza kwa mazingira bora ya uwekezaji Afrika.

Alisema kati ya miradi hiyo iliyosajiliwa, asilimia 35 inamilikiwa na watanzania, asilimia 41 ni ya wageni na asilimia 24 ni ya ubia kati ya watanzania na wageni.

Kuanzia Machi 2021 hadi Machi, mwaka huu, alisema TIC imesajili miradi 1,188 sawa na ongezeko la asilimia 63.19 ikilinganishwa miradi 728 iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho, Machi 2018 hadi Machi 10, 2021.

Alisema kwenye ajira zilizozalishwa kutokana na usajili wa miradi kumekuwa na ongezeko la asilimia 231.63 kutoka ajira 104,172 zilizozalishwa kipindi cha miaka mitatu ya kuanzia mwaka 2018 mpaka 2021 mpaka ajira 345,464 zinazotarajiwa kuzalishwa katika kipindi cha miaka mitatu ya awamu ya sita kuanzia Machi 2021 mpaka Machi 2024.

Teri alisema kumekuwa na ongezeko la usajili wa miradi kutoka nje linatokana na juhudi zinazofanywa na Rais Samia katika kuitangaza nchi na kuhamasisha uwekezaji kupitia sera maalum ya ushirikano kupitia Diplomasia ya Uchumi.

Alisema ongezeko la miradi linatokana na ushiriki wa Tanzania katika makongamano mbalimbali nje ya nchi na maboresho mbalimbali yanayofanywa na Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini

Teri alisema tathmini inaonyesha kuwa idadi kubwa ya miradi iliyosajiliwa iko katika sekta ya uzalishaji viwandani (538), usafirishaji (225), utalii ( 110), ujenzi wa majengo ya biashara (106) na kilimo miradi 106. Alisema Tanzania inaendelea kuwa kinara Afrika Mashariki katika kupokea wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini na kwamba hiyo imetokana na mabadiliko yaliyofanywa kwa kuleta sheria mpya na bora ya uwekezaji ya Tanzania ya mwaka 2022.

Mkurugenzi huyo alisema sheria za uwekezaji zina nafasi muhimu katika kuboresha mazingira ya biashara na kuchagiza wawekezaji kwani imeweza kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja FDI zaidi nchini Tanzania.

Alisema vivutio vya kikodi na sheria mpya za uwekezaji zinatoa vivutio mbalimbali vya kikodi na visivyokuwa vya kodi ili kuhamasisha uwekezaji wa ndani na wa kigeni na kwamba vivutio hivyo vinajumuisha vivutio vya kodi kwa wawekezaji wa kawaida na wa kimkakati.

Teri alisema matarajio ya TIC kwa mwaka wa 2024, ni kusajili miradi 1,000 ya uwekezaji, katika kipindi cha msimu wa 2024 na kuweka malengo ya kuvutia mitaji ya kigeni yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni tano na kuvutia mitaji ya ndani ya

# DC aagiza uchunguzi shughuli wawekezaji

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MKUU wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash, ameagiza viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji kuchunguza na kufahamu shughuli zinazofanywa na wawekezaji kwenye maeneo yao.

Okash alisema hayo juzi kwenye kliniki ya kusikiliza kero katika kata ya Kiwangwa wilaya ya Bagamoyo ambayo ameianzisha kwa ajili ya kuwapatia ufumbuzi wananchi kero zinazowakabili kwenye maeneo yao ikiwamo migogoro ya ardhi.

Katika mkutano huo, iliibuka sintofahamu kwa wananchi kumwomba mkuu wa wilaya kuingilia kati mgogoro kati ya wananchi wa kitongoji cha Misani, kijiji cha Kiwangwa na mwekezaji Kenneth Mwemsi, anayemiliki kampuni ya Sunup.

Mkuu huyo wa wilaya aliagiza Idara ya Ardhi ya Halmashauri ya Chalinze, Ofisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza uhalali wa umiliki wa maeneo ya mwekezaji huyo kwa kukagua nyaraka za ununuzi.

"Mwekezaji huyu amenunua maeneo mengi na hatujui amenunuaje. Chunguzeni mikataba yake na mtusaidie kujua uwekezaji anaofanya ili kuondoa hii sintofahamu iliyopo sasa," alisema.

Okash alisema katika mkutano huo kero nyingi ambazo zingine zilikuwa zipelekwe mahakamani ziko ambazo zimepatiwa ufumbuzi wa papo kwa papo kutokana na kuwa na wataalamu wa idara husika pamoja na mwanasheria.

Mkuu wa Idara ya Ardhi wa Halmashauri ya Chalinze, Deo Msilu, alisema katika kliniki hiyo, mashauri 30 ya wakulima na wafugaji walijitokeza kuhusu eneo la Misani.

Alisema migogoro ya ardhi hasa katika halmashauri hiyo inachangiwa na ongezeko la watu na ungiaji holela kwa jamii ya wafugaji

Mmoja wa wananchi waliokuwa wakilalamikia eneo lao kuchukuliwa na mwekezaji, Morani Mbambarai, alimshukuru mkuu wa wilaya kwa kuanzia utaratibu huo ambao utasaidia kupata majibu kwa haraka na kutatuliwa kero zao kwa wakati.

Mbambarai alisema kwa muda mrefu walikuwa wakilalamikia eneo lao kuchukuliwa na mwekezaji huyo na kutokana na hatua aliyochukua mkuu huyo wa wilaya ya kuagiza uchunguzi kufanyika imeleta matumaini kwa wananchi hao.

Paulo Samnyesi, aliomba serikali iwasaidie kuwapatia maeneo mbadala ili waendelee na shughuli zao za ufugaji tofauti na walipo sasa ambayo mengi yanetwaliwa na Mwekezaji huyo.

Kuhusu tuhuma zilizotolewa dhidi yake, Mwemsi alisema amekuwa alinunua maeneo katika vijiji vya Mwavi na Kiwangwa tangu mwaka 2012 kupitia kwa wananchi moja kwa moja na vielelezo vyote vya kumiliki anavyo.

"Tuhuma zote si za kweli. Wengi wanaolalamika hawana nyaraka na nimekuwa nikifuata taratibu za ununuzi zinazotakiwa na kutokana na agizo la mkuu wa wilaya, natarajia kupeleka vielelezo vinavyotakiwa sehemu husika," alisisitiza.

# UJUMBE WA MHESHIMIWA PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB), WAZIRI WA UCHUKUZI KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA HALI YA HEWA DUNIANI (WORLD METEOROLOGICAL DAY - WMD)", 23 MACHI, 2024

*Ndugu wanahabari,*

Mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi yameendelea kuwa ni mojawapo ya changamoto kubwa katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu kidunia, kikanda na hata katika Taifa mojamoja ikiwemo Tanzania. Kasi ya ongezeko la joto imeendelea kuwa kubwa hususan katika miaka kumi (10) iliyopita. Tayari madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi yanaonekana na yatakuwa makubwa zaidi tusipochukua hatua stahiki sasa. Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) ni mojawapo ya Taasisi yenye mchango mkubwa katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi kupitia utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa sekta zote za kiuchumi na kijamii. Hapa kwetu Tanzania, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imepewa jukumu hilo kisheria la kutoa, kuratibu na kudhibiti huduma za hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kuchangia katika jitihada za Taifa za kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi.

*Ndugu wanahabari,*

Siku ya Hali ya Hewa Duniani ni kumbukizi ya kuanza kutumika kwa Mkataba wa kuanzishwa kwa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) mnamo tarehe 23 Machi 1950. Hivyo, Siku ya Hali ya Hewa Duniani husherehekewa kila ifikapo tarehe 23 Machi ya kila mwaka kwa kuongozwa na ujumbe wa Kaulimbiu. Kaulimbiu ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani kwa mwaka huu wa 2024 iliyopitishwa na nchi wanachama wa WMO, ni "At the frontline of climate action". Kwa tafsiri inasema "Kuwa Mstari wa Mbele Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi".

*Ndugu wanahabari,*

Lengo la Kaulimbiu hii ni kuhamasisha na kuchukua hatua stahiki za kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi ambapo, moja ya hatua hizi kubwa ni kuimarisha mchango muhimu wa huduma za hali ya hewa kwa usalama na ustawi wa jamii.

*Ndugu wanahabari,*

Lengo la 13 la Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goal 13-Climate Action) linasisitiza nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa "kuchukua hatua za haraka kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi; na athari zake." Utekelezaji wa lengo hili unachagiza maendeleo na mafanikio ya Malengo mengine yote ya Maendeleo Endelevu. Vilevile, "Mpango wa Umoja wa Mataifa wa utoaji wa tahadhari kutokana na hali mbaya ya hewa kwa jamii yote-(Early Warning for All-EW4All)" uliozinduliwa rasmi na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Novemba, 2022 unatoa wito kwa Ulimwengu mzima kufikiwa na mpango huu wa tahadhari yaani EW4ALL ifikapo mwishoni wa mwaka 2027.

*Ndugu wanahabari,*

Kaulimbiu ya siku ya hali ya hewa Duniani na shughuli zitakazofanyika kwa mwaka huu 2024 zinalenga kuhamasisha utekelezaji kwa vitendo wa mipango hii ya EW4ALL na Lengo la 13 la Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu, pamoja na utekelezaji wa mipango na mikakati mingine.

Ndugu wanahabari,


Katika kuadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani, Tanzania kama Mwanachama wa Shirika la hali ya Hewa Duniani na Umoja wa Mataifa haijabaki nyuma katika kuchukua hatua Madhubuti kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi kwani yameendelea kuathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kilimo, ujenzi, utalii, miundombinu, usafirishaji, nishati na afya. Mifano ya hivi karibuni ni mvua kubwa zilizochagizwa na uwepo wa El Nino na kusababisha vifo na uharibifu wa miundombinu hasa barabara na nyumba za watu.

*Ndugu wanahabari,*

Hatua zilizochukuliwa na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukabiliana na janga hili la mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, ni pamoja na uboreshaji wa huduma za hali ya hewa na uimarishaji wa mfumo wa utoaji tahadhari (Early Warning Systems) nchini. Uboreshaji huu pia ni sehemu ya utekelezaji wa ILANI ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Ibara ya 59 J ikiweka malengo ya kuimarisha miundombinu na huduma za hali ya hewa nchini. Aidha, uboreshaji huu pia ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma za hali ya hewa ili kufika kwa jamii katika ngazi zote nchini-National Framework for Climate Services-NFCS" kwa lengo hilohilo la kukabiliana na kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na kuhakikisha usalama wa chakula na afya pamoja na matumizi bora ya vyanzo vya maji.

*Ndugu wanahabari,*

Katika kuboresha huduma za hali ya hewa na tahadhari za hali mbaya ya hewa nchini, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya hali ya hewa ikiwa ni pamoja na ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kisasa ya upimaji na uchakataji wa taarifa za hali ya hewa, ikiwa ni pamoja na kompyuta kubwa ya kisasa na yenye uwezo mkubwa wa kuchakata data za hali ya hewa. Kompyuta hii inaiwezesha TMA kuboresha na kuongeza usahihi wa utabiri wa hali ya hewa hususan kwa maeneo madogomadogo, ambapo huduma hiyo imeshaanza kutolewa hadi ngazi ya wilaya kwa utabiri wa mvua za msimu.



WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI - PROF. MAKAME MBARAWA

*Ndugu wanahabari,*

Aidha, Serikali iko hatua za mwisho kukamilisha mtandao wa jumla ya Rada saba (7) za hali ya hewa, ambapo katika kipidi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya sita, malengo ya ununuzi wa Rada nne (4) yamefikiwa. Kati ya hizo Rada mbili zinakamilishwa kufungwa katika mikoa ya Mbeya na Kigoma na utengenezaji wa rada nyingine mbili (2) zitakazofungwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Dodoma unaendelea kiwandani nchini Marekani na zinatarajiwa kukamilika na kufungwa mwaka huu wa 2024. Rada nyingine tatu (3) zimekamilika na kufungwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Mtwara. Hatua hii inaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza Kikanda (Afrika Mashariki) kuwa na idadi kubwa ya rada za hali ya hewa na kuimairisha huduma za uangazi na utabiri wa matukio ya hali mbaya ya hewa.

*Ndugu wanahabari,*

Vilevile, Serikali imetambua changamoto kubwa iliyopo kwa baadhi ya maeneo yanayoathirika na radi za mara kwa mara na imenunua seti tano (5) za vifaa vya utambuzi wa matukio ya radi (Lighting detectors) ambavyo vimefungwa katika maeneo ya Musoma, Mwanza, Kagera (Bukoba), Tabora na Kigoma (Kibondo).

*Ndugu wanahabari,*

Kwa kutambua kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu, Serikali imewezesha ununuzi wa vituo kumi na tano (15) vya kupima hali ya hewa vinavyojiendesha vyenyewe (Automatic Weather Stations) ambavyo vitafungwa katika vituo vya utafiti na maendeleo ya kilimo ili kuchagiza utafiti kuhusiana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa sekta ya kilimo.

*Ndugu wanahabari,*

Katika kuimarisha huduma za hali ya hewa kwa ajili ya usafiri wa anga, Serikali imeendelea kuwekeza katika kuimarisha mtandao wa vituo na uwezo wa uchakataji taarifa, ikiwemo ununuzi na ufungwaji wa vifaa vya kisasa vya hali ya hewa vinavyojiendesha vyenyewe (AVIMET) vinavyosaidia kutoa taarifa sahihi za hali ya hewa kwa ndege zinaporuka na kutua.

*Ndugu wanahabari,*

Hatua nyingine zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ni pamoja na ujenzi wa Kituo cha hali ya hewa na ufuatiliaji wa Tsunami cha Kanda ya Mashariki, Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuimarisha ufuatiliaji wa matukio ya hali mbaya ya hewa hususan yanayoanzia baharini na ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 39.

*Ndugu wanahabari,*

Uboreshaji huu wa miundombinu unaenda sambamba na kuwajengea uwezo wataalamu wa hali ya hewa na watumishi katika sekta hii na wameendelea kupatiwa mafunzo mbalimbali ambapo katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya sita jumla ya watumishi 228 (Wanaume 177 na Wanawake 51) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya diploma (33), shahada ya kwanza (90), Shahada ya Uzamili (79) na Shahada ya Uzamivu (16) kupitia vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi.

*Ndugu wanahabari,*

Katika duru za kimataifa, kwa kutambua mchango wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, tarehe 06 Septemba 2023 wakati wa Kongamano la 23 la Afrika la masuala ya hali ya hewa na tabianchi (African Climate Summit 23) lililofanyika Nairobi, Kenya Mheshimiwa Rais aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Kituo cha Dunia cha Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabia nchi (Advisory Board of the Global Centre on adaptation). Vilevile, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt. Ladislaus B. Chang'a alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (Intergovernmental Panel on Climate Change - IPCC) katika uchaguzi wa viongozi wapya wa IPCC uliofanyika tarehe 26 Julai 2023, Nairobi Kenya wakati wa Mkutano wa 60 wa IPCC; Ikumbukwe kuwa pia hapo nyuma aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa TMA Dkt.Agnes Kijazi, alishawahi kuchaguliwa kushika nafasi ya juu ya uongozi wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) ya kuwa Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika hilo (2019-2022). Hii ni heshima kubwa kwa nchi yetu katika juhudi za kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi Nchini na Duniani kwa ujumla.

*Ndugu wanahabari,*

Haya ni baadhi tu ya mafanikio machache kati ya mengi ambayo yanatokana na Serikali kuendelea kuchukua hatua za kuboresha na kuimarisha huduma za hali ya hewa hapa nchini kwa kutenga fedha katika bajeti ya Maendeleo ya kila mwaka.

Serikali inathamini kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) katika kutoa huduma na taarifa za hali ya hewa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi nchini. Aidha, natoa rai kwa wadau mbalimbali wa maendeleo na mashirika ya Serikali na yasiyo ya kiserikali kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuboresha huduma za hali ya hewa.

*Ndugu wanahabari,*

Mwisho, nawakumbusha na kuwasisitiza wananchi na WADAU wote wa hali ya hewa kuendelea kutumia ipasavyo taarifa za hali ya hewa kwa kuzingatia miongozo na Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya mwaka 2019.

"Kuwa Mstari wa Mbele Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi"

***Siku ya Hali ya Hewa Duniani - 2024***

**Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (MB)**
**Waziri wa Uchukuzi**

## SIKU YA HALI YA HEWA DUNIANI -2024

# UJUMBE WA KAIMU MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA (TMA), MWAKILISHI WA KUDUMU WA TANZANIA KATIKA SHIRIKA LA HALI YA HEWA DUNIANI (WMO), NA MAKAMU MWENYEKITI WA JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI (IPCC), DKT. LADISLAUS BENEDICT CHANG'A KATIKA SIKU YA HALI YA HEWA DUNIANI, TAREHE 23 MACHI, 2024

Leo ni Siku ya Hali ya Hewa Duniani. Jumuiya ya Hali ya Hewa Duniani huadhimisha Siku ya Hali ya Hewa kila ifikapo tarehe 23 Machi tangu kuanzishwa kwa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na kuanza kutumika kwa Mkataba ulioanzisha WMO mnamo tarehe 23 Machi 1950.

Maadhimisho haya huonesha mchango na umuhimu wa Taasisi za Kitaifa zinazotoa huduma za hali ya hewa kwa usalama na ustawi wa jamii. Tanzania ikiwa ni miongoni mwa Nchi 193 wanachama wa WMO inaungana na Jumuiya ya Kimataifa kuadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani na kuonesha dhamira yake ya kuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi.

Kaulimbiu ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani kwa mwaka 2024 ni "Kuwa Mstari wa Mbele Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi". Kaulimbiu hii ilichaguliwa kwa kuzingatia lengo la 13 la Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goal 13-Climate Action) ambalo linaitaka jamii kuchukua hatua za haraka kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Mpaka sasa, mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi yameathiri kila nchi katika kila bara na pia tunatambua kuwa ripoti za Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC) zinaangazia kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la joto ambalo halijawahi kushuhudiwa sambamba na kuongezeka zaidi kwa matukio ya hali mbaya ya hewa na athari zake. Athari hizi zinazidi kuongezeka na kusababisha changamoto mbalimbali katika uchumi wa taifa na kuathiri maisha ya kila siku na hata ya baadae. Aidha, kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi chafuzi kunakotokana na shughuli za viwanda kumesababisha wastani wa joto duniani kupanda zaidi ya nyuzi joto moja (1°C) ikilinganishwa na viwango vya mwaka 1850 - 1900. Kwa upande mwingine, mwaka 2023 ulivunja rekodi kwa kuwa mwaka wenye joto zaidi katika historia ya dunia ukichagizwa na ongezeko la gesijoto na uwepo wa hali ya El Niño. Wastani wa ongezeko la joto kidunia kwa mwaka 2023 ulkuwa nyuzi joto 1.4 °C ikilinganisha na kipindi cha kabla ya mapinduzi ya viwanda. Kwa upande wa Tanzania ongezeko la joto kwa mwaka 2023 lilifikia nyuzi joto 1.0 OC. Ongezeko hili kubwa likiambatana na matukio ya hali mbaya ya hewa, ikiwemo mvua kubwa, mafuriko na upepo mkali vimechangia kuleta maafa ikiwemo vifo na uharibifu mkubwa wa mali na miundombinu.

Kwa muktadha huo, WMO na Wanachama wake wanaweka vipaombele vya kuimarisha huduma za hali ya hewa sanjali na kuelimisha jamii kuhusu matumizi stahiki ya huduma na taarifa za hali ya hewa.

Huduma za hali ya hewa zinazotolewa nchini Tanzania zimeendelea kuwa bora zaidi katika historia ya nchi yetu kabla na baada ya uhuru. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya uwekezaji mkubwa katika ununuzi na uboreshaji wa miundombinu ya uangazi sambamba na wafanyakazi kujengewa uwezo. Maboresho hayo ni pamoja na ufungaji wa vifaa vya kisasa vya kuhakiki utendaji kazi wa vifaa vya hali ya hewa (Calibration Laboratory Equipments), rada za hali ya hewa, vifaa vya utambuzi wa matukio ya radi (Lightning detector) na kompyuta yenye uwezo mkubwa wa kuchakata data za hali ya hewa (Computer cluster). Uwekezaji huu umeongeza kwa kiasi kikubwa ubora na usahihi wa taarifa za utabiri wa hali ya hewa na tahadhari za mapema hadi kufikia wastani kati ya asilimia 80 hadi 98 juu ya asilimia 70 inayokubalika kimataifa. Hii inazifanya huduma za TMA nchini kuwa za uhakika na kuchangia kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi sambamba na kuokoa maisha na mali kutokana na matukio ya hali mbaya ya hewa.

TMA inaendelea kuwa mstari wa mbele kutoa mchango katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi kwa kutfanya tafiti na kuhamasisha matumizi ya sayansi na uvumbuzi miongoni mwa wataalamu wake na wataalamu wengine katika vyuo vikuu na taasisi za utafiti nchini na barani Afrika. Wataalamu wa TMA wameendelea kubuni mifumo mbalimbali ya kuongeza ufanisi na kuimarisha uchakataji wa data na utoaji wa huduma za hali ya hewa. Mifumo hiyo ni pamoja na; TMA Digital Meteorological Observatory (DMO) ambao hutumika katika kuimarisha mawasiliano ya data za hali ya hewa kutoka vituoni kote nchini; mfumo wa utoaji wa taarifa za hali ya hewa kwa watumiaji wa bahari na maziwa (Meteorological Marine MMAIS) na mfumo wa "Meteorological Aviation Information System (MAIS)" ambao hutumika katika mawasiliano na sekta ya usafiri wa anga. Mifumo hii imekuwa na manufaa na kuleta tija kubwa katika mawasiliano ya taarifa za hali ya hewa kwa watumiaji wa huduma za hali ya hewa ikiwemo sekta ya anga na baharini. Huduma za hali ya hewa kwa ajili ya sekta ya usafiri wa anga nchini zimethibitishwa na zinatumbuliwa kukidhi vigezo na viwango vya kimataifa kwa mujibu wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO) kwa cheti cha ISO 9001:2015 tangu mwaka 2017 na kabla ya hapo ISO 9001:2008.



**Dkt. Ladislaus Benedict Chang'a**
***KAIMU MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA (TMA);***

Katika hatua ya kuimarisha utoaji na matumizi ya huduma za hali ya hewa na kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, Serikali ilitunga Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya mwaka 2019. Pamoja na utoaji wa huduma za hali ya hewa, Sheria inaiagiza TMA kusimamia na kuratibu huduma za hali ya hewa nchini. Hii inajumuisha usajili na ukaguzi wa vituo vyote vya hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusimamia data zote za uangazi wa hali ya hewa. Ni kosa kisheria kuwa na kituo cha hali ya hewa ambacho hakijasajiliwa. Lengo ni kuendelea kuimarisha upatikanaji wa takwimu za uangazi zenye ubora ili kusaidia uboreshaji wa huduma za hali ya hewa pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na pia kuongeza kiasi cha data kupitia Mfumo wa Mawasiliano wa data na taarifa za hali ya hewa Kimataifa wa WMO (Global Telecommunication System) na ule wa WMO Information System (WIS).

Ili kuwa na idadi kubwa ya wataalam wabobevu na wenye uwezo katika taaluma ya utabiri wa hali ya hewa pamoja na uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, ni muhimu pia kuendelea kuwajengea uwezo wataalam waliopo na wanaochipukia wa hali ya hewa na wale wa mazingira. Hivyo, TMA inamiliki na kuendesha Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa (National Meteorological Training Centre, NMTC) kilichopo mkoani Kigoma (www.nmtc.ac.tz). NMTC inatoa mafunzo ya hali ya hewa kwa ngazi ya cheti (NTA Level 4) na astashahada (NTA Level 5 na 6). Jukumu la NMTC ni kukuza uwezo wa wataalamu katika nyanja ya sayansi ya hali ya hewa ndani na nje ya Tanzania. Miongoni mwa moduli zinazofundishwa ni uangazi na utabiri wa hali ya hewa, matumizi ya satellite na rada za hali ya hewa katika utabiri wa hali ya hewa (remote sensing, radar meteorology), mabadiliko ya tabianchi na sayansi nyingine zinazohusiana ikiwa ni pamoja na uratibu na usimamizi wa mazingira. Aidha, Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa (NMTC) kimesajiliwa kwa nambari REG/EOS/025 mnamo Machi 2014 na kuthibitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Hivyo, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uwekezaji mkubwa wa kuimarisha miundombinu ya huduma za hali ya hewa na kuendelea kuijengea uwezo TMA kitaasisi na kiufundi na kuifanya Tanzania kuwa mojawapo ya nchi ya mfano katika ubora wa huduma za hali ya hewa katika Afrika na katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani.

Huduma zinazotolewa na TMA ni pamoja na utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku tano, siku 10, mwezi, msimu na tahadhari za mara kwa mara za hali mbaya ya hewa pamoja na mwelekeo wa mvua za msimu katika maeneo madogo hadi ngazi ya Wilaya. TMA pia inatoa taarifa za hali ya hewa ikiwemo taarifa ya kila mwaka ya hali ya hewa ya Tanzania (Statement on the Status of Tanzania Climate) tangu mwaka 2011. Taarifa za hali ya hewa zinapatikana kwa urahisi kwenye tovuti ya TMA (www.meteo.go.tz) ilhali taarifa nyingine mahsusi hupatikana kwa mteja kutuma rasmi maombi TMA ya kupatiwa taarifa hizi. Katika kuhakikisha taarifa za hali ya hewa zinawafikia watumiaji wote, TMA imeendelea kuboresha mifumo ya usambazaji wa taarifa hizo kwa kutumia njia mbalimbali za usambazaji ikiwemo tovuti ya TMA, barua pepe, televisheni, redio za jamii, magazeti, mitandao ya kijamii na simu za mkononi. TMA pia ina programu za kuifikia jamii wakiwemo wanafunzi ili kuongeza uelewa juu ya sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na athari zake na mipango ya kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na upandaji miti, umuhimu na matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na TMA katika shughuli zao za kila siku.

Katika kuadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani 2024, natoa rai kwa wadau wote kushiriki katika kujenga uelewa na kutumia ipasavyo taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na TMA ili kuendelea kuongeza tija na ufanisi katika kupanga na kutekeleza shughuli zetu za kijamii na kiuchumi, na kuchangia katika kuokoa maisha ya watu na mali zao kutokana na changamoto ya matukio ya hali mbaya ya hewa. Pia tunaendelea kuwakumbusha wadau wote kufuata na kuzingatia Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya mwaka 2019 na kanuni zake ili kuhakikisha uendelevu na ufanisi wa huduma za hali ya hewa nchini Tanzania.

**Nawatakia maadhimisho mema ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani 2024**

**""Kuwa Mstari wa Mbele Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi"."**

***Siku ya Hali ya Hewa Duniani -2024***

Dkt. Ladislaus Benedict Chang'a
KAIMU MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA (TMA); MWAKILISHI WA KUDUMU WA TANZANIA KATIKA SHIRIKA LA HALI YA HEWA DUNIANI (WMO); NA MAKAMU MWENYEKITI WA JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI (IPCC)





## SMZ kumlinda mtumiaji mazingira

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesisitiza kuwa itaendelea kusimamia sheria na kanuni katika kumlinda mtumiaji na mazingira kuhakikisha uzalishaji wa bidhaa unalindwa

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Sharif Ali Sharif wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Viwango Afrika yaliyofanyika Kikwajuni mjini Unguja.

Sharif alisema hatua hiyo itaziwezesha bidhaa zinazozalishwa Zanzibar kuhimili ushindani katika masoko ya nje, kuimarisha biashara na kujitangaza kitaifa na kimataifa.

Alipongeza uamuzi wa Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) kushirikisha wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu kwenye uandishi wa insha zenye mada zinazohamasisha umuhimu wa viwango, kwa kuwa vyuo vina mchango mkubwa kukuza uelewa wa jamii.

Alisema vyuo vinafanya tafiti ya utumiaji wa bidhaa, kubaini athari na faida za bidhaa zisizo na viwango na kuwataka wakuu wa vyuo kuwahamasisha wanafunzi kufanya tafiti ili kuwa mabalozi wazuri kwa jamii.

"Hatua ya kuwashirikisha vijana kunatoa fursa ya wanafunzi kuchanganua mawazo yanayolikabili taifa chini ya kauli mbinu isemayo; 'Kuwawezesha watumiaji kwa kuwapatia viwango ili kupata haki zao za huduma zenye ubora na salama," alisema Waziri Sharif.

Mkurugenzi wa Biashara na Masoko wa Wizara wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Khamis Ahmada Shauri, alisema wafanyabiashara wamehamasika kuthibitisha biashara zao kupitia ZBS na kuimarisha maendeleo ya biashara nchini.

Shauri alisema wzara hiyo imeridhiswa na utendaji kazi wa shirika hilo kwa kusaidia upatikanaji masoko ya bidhaa zinazothibitishwa na kuyafikia masoko ya ndani na nje ya nchi.

Aliipongeza ZBS kwa kudhibiti uingizaji wa bidhaa zisizokuwa na viwango visiwani hapa kwa kutoa elimu kwa wafanyabishara, waingizaji na watoaji wa bidhaa.

Mkurugenzi Mkuu wa ZBS, Yussuph Majid Nassor, alisema wamekuwa wakitoa elimu ya viwango kwa makundi mbalimbali wakiwemo wanafunzi.

Alisema katika maadhimisho hayo, wanafunzi 93 kutoka vyuo mbalimbali wameshiriki katika shindano la insha kwa lengo la kumpata nshindi wa kwanza ambaye ataiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kikanda.

Katika shindano hilo la 11, ZBS ilikabidhi vyeti, fedha na zawadi kwa wanafunzi watano baada ya kuibuka washindi.

# Walimu waonywa ufundishaji kizamani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imeonya haitakuwa tayari kuona mwalimu anaendelea kutumia mbinu za kizamani za ufundishaji ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne.

Onyo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Lela Muhammed Mussa wakati akikabidhi vyeti kwa zaidi ya walimu 2,276 wa sekondari na maofisa elimu baada ya kuhitimu mafunzo ya umahiri ya kuboresha elimu na kuinua kiwango cha ufaulu visiwani hapa.

Mussa alisema kuwa mafunzo hayo yalitolewa kupitia Mradi wa EQSE-Z kwa ufadhili wa Shirika la Koica na Good Neighbors, yatawasaidia kuboresha mazingira ya ufundishaji, uwezo wa walimu kutekeleza mbinu za umahiri na kuimarisha uwezo wa kamati za shule na jamii kushiriki kufuatilia ubora wa maendeleo ya elimu.

Alisema mafunzo hayo yataongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa kidato cha nne kwa masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza.

Mussa alisema utekelezaji wa miaka mitatu ya mradi huo kuanzia mwaka 2022 wa mafunzo kazini kwa walimu, umewajengea uwezo na mbinu za kusimamia mitaala ya elimu wa umahiri ili kupata matokeo mazuri ya kidato cha nne.

Alisema kupata mafunzo ni jambo moja na utekelezaji ni jingine na kuwataka walimu hao kubadilika kutoka katika mfumo wa awali wa ufundishaji wa kuhariri maudhui na kuanza kutumia mbinu mpya za umahiri ili wanafunzi wawe kitovu cha ufundishaji.

Aliwataka walimu kubadilika kwa kuwa ndio mwelekeo mpya wa elimu, sera na mageuzi ya elimu yalioridhiwa na serikali inayoongozwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi kutumia mtaala mpya.

Alisema katika maboresho ya mitaala mipya ambayo utekelezaji wake unafanyika kwa awamu, umahiri kwa wanafunzi na elimu ya ufundi vimetiliwa mkazo, hivyo asiyetaka kubadilika atajikuta yupo nje ya mfumo na wizara hiyo haitakuwa tayari kuona mwalimu atakayeendelea kutumia mbinu za kizamani za ufundishaji.

Waziri huyo aliwataka maofisa elimu, wakuu wa shule na waratibu wa vituo vya mafunzo ya walimu kuanzisha na kusimamia uratibu wa mafunzo kazini ngazi ya shule na kuweka kumbukumbu za walimu wanaoshiriki mafunzo hayo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Khamis Abdalla Said, aliwapongeza walimu kwa kuleta mabadiliko ya ufaulu wa wanafunzi hasa wa sayansi.

Kwa mujibu wa Said, uongozi wa wizara hiyo unatarajia mafunzo hayo watayafanyia kazi kwa vitendo na kupata matokeo mazuri ya ufaulu wa wanafunzi.

Alisema wizara hiyo itaendelea kusimamia maslahi ya walimu na kuinua kiwango cha kufundisha wanafunzi na taifa kupata wataalamu bora.

Mratibu wa EQSSEZ, Yejin Cho, alisema mafunzo hayo yataimarisha ubora wa walimu, kuweka msingi imara na kupata maendeleo endelevu ya elimu.

Alisema walimu wakuu 241 wamejengewa uwezo katika masomo ya ufanisi sawa na asilimia 32, waratibu wa mafunzo ngazi ya shule 503 kuratibu mabadiliko chanya kwenye shule zao sawa na asilimia 43 kwa Unguja na Pemba.

Aliahidi wataendelea kushirikiana kusisimua elimu kwa kujenga umahiri wenye fursa wa walimu na wanafunzi visiwani hapa.



Ofisa Mkuu wa Usimamizi wa kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kissa Kyejo (kushoto), akitoa elimu ya kodi kwa mfanyabiashara Emmanuel Mkonya, wakati wa kampeni maalumu ya elimu ya ya mlango kwa mlango wilayani Shinyanga mjini jana, yenye lengo la kuwafikia wafanyabiashara na kuwapa elimu ya kodi na kusikiliza changamoto mbalimbali zinazowakabili na kuzitatua. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watwishwa jukumu kusimamia misitu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo,Umwagiliaji na Maliasili imesema jukumu la usimamizi wa rasilimali za misitu linabaki kwa wananchi na wao ndio watumiaji wakubwa.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Waziri wa Wizara hiyo, Shamata Shaame wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani iliyoambatana na upandaji wa miti katika Kijiji cha Charawe na uzinduzi wa mradi wa mnara wa kimaumbile Shehia ya Pete yaliyofanyika Jonzani, Mkoa wa Kusini Unguja.

Shaame, alisema wananchi wanatakiwa kuendelea kuilinda, kuitunza na kuihifadhi misitu kwa kuwa kutoweka kwake kutawaathiri kwa kiwango kikubwa. "Ningependa kutoa agizo lazima miti tuliyoipanda leo itunzwe vizuri ili misitu iweze kuimarika na kutoa huduma zinazostahiki, pia tunatakiwa tuchukuwe juhudi kubwa tena za makusudi kupanda miti kwa wingi," alisema.

Alisema ikiwa wananchi watapanda miti kwa wingi katika maeneo ya wazi lengo kurejesha Zanzibar ya kijani litafikiwa. Kwa upande mwingine, alikemea uharibifu unaofanywa na jamii wa kukata miti ovyo katika misitu kwa kutumia misumeno ya moto na kusafirisha bila kufuata taratibu.

Akizungumza katika Kijiji cha Charawe wakati wa upandaji miti, Waziri huyo alisema uharibifu wa mazingira umepeleka kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi na kiwango cha joto.

Alionya kuwa atakayekamatwa akihujumu msitu atawajibishwa kisheria bila ya kuonewa huruma.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ali Khamis Juma, alisema utunzaji wa mazingira ni suala mtambuka, hivyo kila mwanajamii anapaswa kushiriki kikamifu ili Zanzibar ibaki salama.



# Wewe unampa ngapi?

MASHABIKI wa muziki nchini wamempongeza mwanamuziki wa Bongo Fleva, Mbosso, kwa kitendo chake cha kuwafuata mashabiki zake na kuwasikiliza matatizo yao.

Hivi karibuni msanii huyo kutoka lebo ya WCB, alikutana na shabiki yake na kumpa zawadi baada ya kumuhadithia mkasa uliomfanya aadhibiwe na mwalimu wake baada ya kukuta daftari lake moja ameandika nyimbo za mwanamuziki huyo.

Mbosso na shabiki huyo walikutana wakati akielekea nyumbani kwake na alipokuwa akikatiza mitaa alimuona kijana huyo na kumtaka dereva wake kusimamisha gari na kupata fursa ya kuzungumza naye machache.

Wakati wa mazungumzo hayo, shabiki huyo alifunguka jinsi alivyokuwa na mapenzi naye kiasi kwamba alihatarisha masomo yake akiwa shuleni kutokana na vitabu vyake vingi alikuwa anaviandika majina na nyimbo za Mbosso.

"Huyu jamaa nishawahi kutana naye, shabiki wangu sana huyu. Kuna siku, sehemu hii hii aliniambia na leo tunakutana tena bana. Mwenyezi Mungu ni mkubwa sana, leo nimemuona tena anapita hapa, njia ile ile, yuko na rafiki zake . Huyu hapa shabiki wangu, nishushie kioo," Mbosso alisikika akimwambia dereva wake.

Walipomaliza mazungumzo hayo, Mbosso aliinama kwenye gari na kuhesabu bunda la noti na kisha kumkabidhi kama zawadi na kuthamini mchango wake katika maisha yake ya kimuziki.

Baadhi ya watu wamekuwa na maoni tofauti kutokana na tukio hilo, huku idadi kubwa wakimpongeza msanii huyo kwa kuwa na moyo wa kijitolea na hasa kwa mashabiki zake.

BASI SAWA

## Vijana wamuandama Omondi



MCHEKESHAJI ambaye amejiingiza katika uwanaharakati nchini Kenya, Erick Omondi, amesema vijana wengi wanaishi bila kuwa na ajira.

Omondi ameonyesha kwenye ukurasa wake wa Instagram ujumbe kutoka vijana 12,000 wa nchi hiyo ambao hakusoma uliotumwa kwake wakiomba ajira.

"Nimepokea jumbe 12,400 kutoka kwa Wakenya wasio na ajira na bado nahesabu!! Niamini tutawatafutia watu hawa ajira. Tutawaunganisha waajiri wa Kenya na wasio na ajira. Tutawasaidia ndugu na dada zetu kupata riziki zao," ameandika.


## KRG ajidai kupendwa Bongo

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya kutoka Kenya, KRG the Don, amejigamba kwamba ana mashabiki wengi Tanzania kuliko nchini mwake.

Akizungumzia ziara yake ya nchini Tanzania ambako alikwenda kumuunga mkono msanii wa Bongo Fleva, Alikiba katika uzinduzi wa kituo chake cha redio, KRG amesema amepata mshangao baada ya kuona ana mashabiki wengi kuliko alivyotarajia.

"Kitu kingine mimi nilienda pale kujumuika na mashabiki wangu, kwa sababu nina mashabiki wengi sana kupitiliza. Sikuwa najua mimi ni mkubwa sana Tanzania hata kuliko hapa Kenya, kusema ukweli Tanzania mimi ni Bughaa sasa, nyinyi mnacheza na Bughaa,"amesema KRG.





# Jacqueline Wolper yanayomkuta mazito

MWIGIZAJI mkongwe nchini, Jaqueline Wolper, amekiri kwamba kwa muda wa miezi kumi hana mawasiliano mazuri na mume wake.

Akizungumza hivi karibuni, Wolper amesema kinachomfanya aendelee kuilinda ndoa yake ni kutokana nakuwa na uvumilivu kama mke na mama mwenye watoto.

"Kuna vitu nilikuwa napitia kwa mume wangu, niwe muwazi katika suala hili toka mwezi wa sita mwaka jana siko sawa na mume wangu lakini kama mke na mama siwezi kila kitu kukiweka hadharani,"Amesema Wolper.



# Zari hana baya kwa Zuchu

MJASIRIAMALI na mwanamke mwenye mvuto mitandaoni, Zarina Hassan, maarufu kama Zari, amesema huwa anaongea vizuri na wapenzi wa mzazi mwenzake, Diamond Platnumz, kama rafiki zake.

Amesema hata Zuchu ambaye ni mpenzi wa sasa wa Diamond, amekuwa akimpigia simu mara kwa mara kupeana taarifa kuhusu watoto wake wakati wanapokuja nchini kumtembelea baba yao.

"Mimi naongea na wanawake wa Diamond bila matatizo, hata Zuchu nazungumza naye kila wakati na hata watoto wakija Tanzania nampigia simu ananiambia maendeleo yao, pale wakikua nitafurahi waishi naye," amesema Zari.

# Endelea kulala pema Kiambukuta

**Na Adam Fungamwango**

NI miaka mitatu sasa tangu dunia ilipoondokewa na mwanamuziki wa dansi la rhumba, mtunzi na mwimbaji mahiri, Josky Kiambukuta, aliyefariki mwezi kama huu, 2021.

Mshtuko mkubwa uliwapata mashabiki wa muziki duniani, baada ya kutoka taarifa za kifo cha mwanamuziki mkongwe nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Josky Kiambukuta.

Alifariki Jumapili ya Machi 7, 2021, akiwa na miaka 72, ambapo wakati wa uhai wake alikuwa mwimbaji kiongozi na mtunzi mahiri wa bendi ya TP OK Jazz iliyokuwa ikiongozwa na Franco Lwambo Lwanzo Makiadi ambaye alifariki dunia mwaka 1989.

Mara ya mwisho alikuwa na kundi la Bana OK, baada ya kifo cha Franco, lakini pia alikuwa akipiga muziki na wakongwe weenzake wakifanya ziara mbalimbali bara la Ulaya, Asia na Afrika.

Ni mwanamuziki aliyeanza kuvuma tangu miaka ya 1960, akiwa na kundi la Africa Fiasta Sukisa lililokuwa likiongozwa na Dk. Nico Kasanda wa Mikalayi.

Alijiunga na TP OK Jazz mwishoni mwa miaka ya 1960 na kujizolea umaarufu mkubwa kutokana na sauti yake tamu, akitunga nyimbo mbalimbali na pia kuimba za wenzake. Katika kumbukumbu ya miaka mitatu, leo tutaziangalia nyimbo tano maarufu kwa mashabiki wa muziki wa dansi ambazo ametunga na kuimba pia.

**Monzo-1974**

Ni moja kati ya nyimbo zilizompatia umaarufu mkubwa na kumpa heshima kubwa kwenye bendi ya TP OK Jazz, chini ya Franco.

'Monzo', ulikuwa ni wimbo maarufu sana katikati ya miaka ya 1970, baada ya kuutunga na kuutoa mwaka 1974, ukipigwa kila kona, hata hapa nchini Tanzania.

Gitaa kali staili ya 'kente', ilichangia wimbo huo kupendwa sana na mashabiki.

**Fariya-1977**

Mwaka 1977, alikuja na kibao kimoja alichokiita 'Fariya' ambacho nacho kilizidi kumfanya kuwa mmoja wa wanamuziki tegemeo na wenye heshima kubwa kwenye bendi hiyo, licha ya kwamba kulikuwa na waimbaji wengi kwenye bendi hiyo.

**Missile-1983**

Jamaa alikuwa habahatishi. Mwaka 1983, aliibuka na kibao kingine kilichopendwa sana kilichokuwa na jina la 'Missile'.

Kilipigwa na staili ya taratibu, lakini kinachopendeza mno masikioni, pamoja na yenye mwenyewe kuimba kwa huzuni, akighani kwa hisia kali sana, huku gitaa likipigwa kwa kubembeleza.

**KSK-1984**

Mwaka mmoja baadaye alitunga wimbo mmoja ulitwao 'KSK' na kuzidi kujijengea heshima ya kuwa mwimbaji mwandamizi kwenye bendi hiyo.

**Chadra Dechade-1989**

Huu ndiyo mwaka ambao Franco alifariki. Na ndiyo mwaka ambao alitoa kibao maarufu sana kiitwacho 'Chandra Dechade.'

Hadi leo huwa kinapigwa kwenye bendi nyingi zinazopiga muziki wa laivu. Ni moja kati ya nyimbo zake ambazo zilinyanyasa sana mwanzoni mwa miaka ya 1990, hadi leo hii ukipigwa, watu wanaacha viti vyao. Madilu Sytem pia ana kipande chake alichoimba kwenye wimbo huu.






# Ndoa ndoana kijana

**Na Adam Fungamwango**

NDOA zina changamoto nyingi sana, ndiyo maana wazazi wengine wanaruhusu watoto wao kuoa au kuolewa akili zinapokomaa na si mwili au umri.

Baadhi ya vijana hufikiri upande mmoja tu wa raha, lakini unapokuja upande wa tabu inakuwa matatizo. Hapo ndoa inakuwa tafrani, na ndipo unapokuja ule usemi usemao, 'ndoa ndoana.'

Hii tunaiona katika filamu ya 'Ndoa Ndoana', ambapo mtunzi ameangazia eneo moja la changamoto katika ndoa.

Rehema Mtonyi, Ismail Ramadhani, Mariam Rashid, Hugo Wangoma, ni baadhi ya waliocheza filamu hiyo.

Salama ni mke wa Tata. Anapigwa na mumewe kwa kosa la kuweka chumvi nyingi kwenye mboga.

Kipigo kinamfanya kukimbilia kwao ambako nako wazazi wake wanamtimua, wakitaka arudi kwa mumewe, au arejee kwao akiwa na talaka tatu mkononi.

Salama anarejea kwa mumewe na kuomba msamaha. Hata hivyo bado haumzuii mumewe kuendelea kumpa vipigo na manyanyaso kibao.

Kisa kikubwa ni kwamba mkewe hazai. Ana miaka kibao anaishi naye bila mtoto.

Tata anaamua kumchukua mwanamke mwingine na kumleta nyumbani kwake mbele mkewe. Mke anawekwa nje. Anabaki analia mlangoni. Ghafla baba yake anatokea. Alikuja kuhakikisha kama kwenye binti yake anateswa kama alivyodai.

Alichokikuta, na kukishuhudia, kilimkera na kuamua kumchukua binti yake akarejea naye nyumbani.

Huku nyuma, kitendo na kuonekana na baba mkwe wake anatoka ndani na mwanamke mwingine, kilichanganya Tata.

Akaanza kumsemea ovyo hawara yake na kumtimua. Anaamua kwenda kuomba msahama kwa mkewe, ananusurika kukatwa mapanga na baba mkwe wake.

Hasira zilipoishwa alipewa nafasi ya kusikilizwa, akaomba msamaha, akakubaliwa huku tayari mkewe akiwa ameshashika ujauzito ambao alitoka nao siku alipochukuliwa na baba yake.



# Teni awapa makavu

MWANAMUZIKI wa Afrobeats kutoka Nigeria, Teni amewaonya watu wanaoomba pesa, kuacha mara moja kwakuwa ni kinyume na utaratibu wa Mungu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Teni amewaita watu hao kama chama cha ombaomba wamekuwa kero kutokana na kutaka pesa kila mara.

"Unaenda kuomba pesa baada ya siku tatu unarudi tena. Je, mimi ni mama yako au baba yako? We chama cha ombaomba mrudie Mungu, si kazi nzuri." Ameandika Teni.



## Mwacheni Solidstar aungame

MSANII maarufu wa muziki wa Afro Beats nchini Nigeria, Solidstar, amesema alijiingiza katika uraibu wa dawa za kulevya bila yeye kupenda.

Akiongea hivi karibuni, msanii huyo ambaye alihamia eneo la Festac katika Jimbo la Lagos baada ya kuishi katika mji wa maraha uliokuwa kisiwani, amesema dawa hizo zilimdhoofisha kiasi ambacho hakuweza kufanya kazi zake.

"Nilipochoka kuishi kisiwani, nilienda Festac kwa sababu nilikuwa kama kichaa. Kule ndiko waliniingiza kwenye matumizi ya dawa na rafiki niliokutana nao," amesema.

## Ariana alipa bil.64 fidia ya talaka

MWANAMUZIKI wa Marekani, Ariana Grande, amejikuta akimlipa aliyekuwa mume wake, Dalton Gomez, Dola milioni 25 sawa Tsh bilioni 64 kama fidia ya talaka.

Kulingana na ripoti ya jarida la The Associated Press, talaka hiyo ilitolewa na Mahakama Kuu ya Los Angele ya nchini Marekani, baada ya ndoa yao kudumu miaka mitatu.

Ariana alidai ndoa yao ilikuwa na tofauti zisizoweza kusuluhishwa na yuko tayari kulipa kiasi hicho mara moja.





## Drake amzawadia shabiki $ 25000

RAPA kutoka Canada ambaye makazi yake yapo Marekani, Drake amemzawadia shabiki wake mjamzito kiasi cha Dola 25000 sawa na Tsh milioni 64 baada ya kumtaka awe baba wa mtoto wake.

Kulingana na jarida la People, alikutana na mwamamke huyo katika tamasha lake lilofanyika kwenye mji wa San Antonio wakati akiendelea na ziara yake ya kimuziki aliyoita 'It's All a Blur'.

Wakati akitoa burudani, Drake aliona bango liloshikiliwa na mwanamke huyo mjamzito kwenye mstari wa mbele, akimtaka msanii huyo awe baba wa mtoto wake.

## Omah Lay kama kunguru

MWANAMUZIKI mkali, Omah Lay, ameibua gumzo baada ya kukataa kucheza na shabiki yake mwanamke jukwaani.

Tukio hilo limekuja siku chache baada ya mwanamuziki huyo kusababisha mjadala nchini Uingereza baada ya kumpandisha jukwaani mwanamke na kuleta mabishano na mpenzi wake.

"Nataka kuchagua msichana kutoka katika umati huu wa mashabiki, lakini sitaki shida naweza hata kucheza na mwanaume mwezangu" alisema na kusababisha mashabiki kupiga kelele za kumshangilia.





## Wanafunzi TGC rasmi HESLB

**Na Frank Monyo,** ARUSHA

HATIMAYE serikali imesikia kilio cha muda mrefu cha Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) kilichopo jijini humo na kukijumuisha rasmi katika orodha ya wanufaika wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Nchini (HESLB).

Jana Kaimu Mratibu wa TGC, Jumanne Shimba alidokeza kuhusu uamuzi huo wa serikali wakati wa kikao kazi na waandishi wa habari walioko kwenye ziara ya kutembelea miradi ya kituo hicho.

"Tunaishukuru serikali baada ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa mwaka wa fedha 2023/24 kuwapokesha wanafunzi 11 mikopo hiyo. Hili tumeliomba kwa muda mrefu na sasa imewezekana," alisema.

Alisema wanafunzi 349 waliohitimu mafunzo ya fani za uongezaji thamani madini kutoka kituo hicho, wamepata fursa za ajira nchini.

"Vijana wengi ambao wamehitimu katika kituo hiki wamepata nafasi ya kuajiriwa na kujiajiri ikiwemo katika kampuni zinazofanya shughuli za uongezaji thamani kutokana na kuwa na ujuzi wa kiwango cha juu," alisema.

Alisema idadi hiyo ya wahitimu ni tangu kituo hicho ambacho kina usajili rasmi wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), kianze kutoa mafunzo mwaka 2015. Shimba, alisema kituo hicho kinatoa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya ukataji na ung'arishaji madini ya vito, fani ya usonara, uchongaji wa vinyago vya vito, utambuzi wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo.

"Sisi tunachowafundisha ni pale madini yanapotoka mgodini kuanza kuyafanyia uchambuzi mpaka pale yanafikia kuwa bidhaa, kuyaongezea thamani hadi kwenda kumfikia mteja," alisema.

Shimba, alisema malengo ya TGC ni kudumisha ubora, viwango, uadilifu na taaluma katika utoaji wa huduma kuhusiana na madini ya vito ili kufikia viwango vinavyotakiwa katika soko la Kimataifa.

## Watoto wenye ulemavu wapatiwa viti vya kisasa

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKATI watu wenye ulemavu wanaotumia viti mwendo bila ushauri wa wataalamu wakitajwa kuwa hatarini kupata madhara ya kupinda mgongo na vidonda mgandamizo vinavyoweza kusababisha kifo kabla ya wakati, Taasisi ya Silver Crescent Fondation, imejitosa kuwapatia viti vya kisasa.

Mratibu wa taasisi hiyo nchini, Kadir Komorcu, alisema wanalo jukumu kubwa la kuwahudumia watoto wenye ulemavu, na kila mtu anayo nafasi kubwa ya kufanya jambo kwa kundi hilo, kwa kuwa tatizo lao ni zaidi ya maisha ya kawaida ya binadamu.

Alisema kutokana na uhitaji huo, wameguswa kutoa msaada wa viti mwendo 10 kwa watoto wenye ulemavu wa viungo wilayani hapa.

Baada ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Wilaya ya Muheza, Dk. Juma Mombokaleo, alisema msaada huo ni muhimu kwao na wa thamani kwa watoto hao.

Vilevile, alisemalicha ya watoto hao kuwa na changamoto hiyo, wazazi wenye watoto wenye ulemavu nao wanapitia changamoto nyingi zaidi katika malezi.

Mwenyekiti kutoka Taasisi ya Tanzania Health Awareness Foundation (TAHAF), Adam Sechonge, alisema watoto hao wenye umri kuanzia miaka mitatu, walikuwa wakikatisha masomo na wengine kushindwa kwenda shule kutokana na kukosa viti vya mwendo.

# Watuhumiwa dawa za kulevya wafurika mahabusu Kilimanjaro

**Na Mary Mosha,** HAI

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini amesema mahabusu za vituo vya Polisi na Magereza mkoani Kilimanjaro zimefurika watuhumiwa wa dawa za kulevya na kuwa tishio kwa nguvu kazi ya taifa.

Sagini aliyasema hayo jana katika Kijiji cha Kwa Sadala kilichoko Wilaya ya Hai wakati akizungumza katika ziara ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango mkoani humo.

Alisema tatizo la matumizi na usafirishaji wa mirungi bado linawaathiri vijana na kusababisha kupotea kwa nguvu kazi hiyo ya taifa.

"Makamu wa Rais, Dk Mpango alisema matukio ya mirungi kwa Wilaya ya Hai na Mkoa wa Kilimanjaro yapo mengi na yanapoteza nguvu kubwa ya taifa kwa kuwateketeza vijana. "Jambo hili limesababisha vituo vya Polisi na Magereza kufurika. Endapo wananchi wakiacha hayo, hawatasumbuliwa na vijana wetu, wala Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Nchini (DCEA)," alisema.

Vilevile alisema Kilimanjaro ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa migororo ya wakulima na wafugaji na kusababisha kukosekana kwa utulivu kwa baadhi ya maeneo.

"Niwaombe chini ya kamati zetu za usalama za wilaya na mkoa, tengeni maeneo na kuimarisha mahusiano mema kati ya wakulima na wafugaji. Ni kweli ni Watanzania wanahitaji huduma, lakini bila usalama shughuli za ufugaji na kilimo haziwezi kufanyika salama," alisema.

Katika hotuba yake, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliagiza viongozi wote wa ngazi za chini kuhakikisha wanatoa elimu dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya ili kupunguza athari zake katika jamii.= "Kwenye chama huko tunapotembelea matawi yetu, viongozi wa dini hakikisheni mnazungumza na vijana juu ya matumizi yoyote ya madawa ya kulevya. Tunataka tuwaache Watanzania vijana kwenye uongozi na sio vijana mazezeta kazi yao kutumia madawa ya kulevya," alisisitiza Dk. Mpango.



Mfadhili wa Taasisi ya Mo Maji Well Drilling Ltd kutoka Saudi Arabia, Mohammed Ainahdi, akiwasaidia akinamama kupika futari, iliyoandaliwa na taasisi hiyo, kwa ajili ya wananchi wa kijiji cha Mafere, wilayani Muheza, mkoani Tanga juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# 'Watanzania tumieni misitu kwa ubunifu'

**Na Ashton Balaigwa,** SAME

KAMISHNA wa Uhifadhi, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Profesa Dos Santos Silayo amesema umefika wakati Watanzania kuanza kutumia misitu kwa mambo ya ubunifu ili kutatatua matatizo ya kidunia.

Prof. Silayo alisema hayo juzi wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro wakati wa kampeni ya upandaji miti kitaifa kwenye taasisi za umma, ikiwemo Shule ya Msingi Same iliyofanyika juzi sambamba na Siku ya Misitu Duniani.

Akizungumzia suala hilo, Prof. Silayo, alisema ubunifu unaozungumziwa ni pamoja na nyanja za kusimamia ardhi na kuendeleza misitu na nyanja za biashara za mazao ya misitu.

Alisema ubunifu huo ni masuala ya teknolojia na sera zinazosimamia rasilimali za misitu kwa kubuni sera na kuleta faida kwa Watanzania.

Vilevile, alisema ubunifu huo uendane na masuala ya utawala na usimamizi ili kuleta tija katika usimamizi wa rasilimali hizo za misitu na kuleta manufaa kwa wananchi .

" Utawala unaozungumziwa ni kama unaofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kupigania uhifadhi wa misitu na usimamizi wa mazingira nchini ili kuifanya Tanzania kuendelea kuwa ya kijani," alisema.

Kuhusu upandaji wa miti, alisema lazima uwe na usimamizi shirikishi na kuimarisha uhifadhi ili miti itakayopandwa ikue na kunufaisha wananchi kwa kuwa wanahitaji zaidi misitu kuliko inavyowahitaji.

"Hapa lazima tukumbuke sisi tunahitaji sana misitu kuliko misitu inavyotuhitaji sisi ili tuweze kupata hewa safi, mvua, kwa kuwa kuna nchi nyingine wanalazimika kurusha maji juu kwa ajili ya kutoa vumbi ili kupata hewa safi lakini sisi bado hatujafikia hali hiyo, hivyo lazima tulinde misitu yetu kwa gharama zozote zile," alisema Prof. Silayo. Balozi wa Mazingira nchini, Ahidi Sinene, alisema katika kuadhimisha Wiki ya Misitu Duniani kazi kubwa wanayofanya ni kuhakikisha mazingira yanatunzwa kwa kupanda miti kwa wingi na kuitunza ili Tanzania iendelee kuwa ya kijani.

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Enzi cha 'chai maharage' ubunifu wa Mwinyi, ulivyokomboa dhiki ya usafiri

**Na Adam Fungamwango**

UNAPOZUNGUMZIA kwa mama ntilie ambao sasa hivi wamepewa promosheni ya jina 'mama lishe', sidhani kama kuna asiyewajua.

Na hilo silo la jana wala juzi, uelewa na watu umekwenda mbali, hata menu ya msosi unaopatikana pale, wanaujua barabara, tena wajuzi hao wanaenda mbali, kujua wali na nazi unapatikana wapi na mbwembwe za mafuta kwenye mboga zinapatikana wapi.

Kikubwa zaidi ni kwenye seti ya hizo menu, zipo nyingi lakini katika tano bora, chai maharage au ubwabwa maharage haukosekani.

Naam, suala la bei tuweke pembani, maana linajulikana kuliko, labda nifanye kukumbushia tu staili ya mkao, ambapo kuna viti vya matofali, mabenchi ya mbao, na mara nyingine, ikiwa hoteli maarufu, isiwe tabu, eneo la wazi kubwa tu, mtu anajidai ubwabwa wake na maharage na wale maalwatan, wana ofa ya kuongezewa mchuzi, matandu au makoko.

Wateja hao wameamka asubuhi, we acha tu, chai ya rangi na yenye tangawizi kwa maharage, tena mekundu, ukipata hayo mbona maisha umeyapatia!

Nakwambia umaarufu wa chai na maharage, wengine tumeanza kuujua tangu wadogo tu wanafunzi, tukiwa tumepigwa marufuku kufika huko, maana swali la kwanza la mzazi, ni hela umepata wapi? Na ukisema



Gari aina ya Canter, ambayo mwanzoni mwa miaka ya 1990, yalitumika kama mabasi ya usafiri Dar es Salaam. Staili ya utengenzaji ukaaji wa kutazamana abiria tofauti na mabasi mengine, yakaitwa 'chai maharage', kufananishwa na jinsi wateja wanavyokaa kwa mama ntilie wakati wakipata msosi.

umepewa chakula cha ofa ndiyo umeharibu kabisa!

Ndani ya umaarufu huo, hakuna asiyejua, seti ya chai na maharage, kuanzia wenzangu na mimi wa uzunguni hadi wa chumba kimoja, chakula kinapikwa kwenye korido, hata kuifanya mlo huo kuwa se-



Jinsi abiria walivyokuwa wakikaa kwenye magari ya usafiri ya 'chai maharage'.

hemu ya kifasihi pori, ambao kila mtu anauelewa. Hilo ndilo somo lililoeleweka vizuri mno hadi kwa wale wanaotufanyia maamuzi kwenye Baraza la Mawaziri, ukimtajia tu hilo anapata picha ya mtu anavyojidai na msosi wake wakitazamana kwenye mabenchi, wakichangia meza moja, maji ya kunawa kwa ujamaa, jagi kubwa la maji ya kunywa lililowekwa barafu, kila mtu akiwa na glasi ya plastiki kujihudumia.

Naam, hizo ndizo zama usafiri wa umma ulikuwa mgumu kweli kweli, usafiri tunaoutegemea, mabasi ya UDA jijini Dar es Salaam, kugombea, kudandia, kusubiri kwa masaa vituoni na huenda ukakosa kabisa! Jamani, tukitamka maendeleo tunamaanisha mengi!

Katika mazingira hayo ndiyo tunamkumbuka sana mzee wetu,

Ali Hassan Mwinyi aliyetutoka hivi karibuni, kwani alisema haiwezekani lazima majibu yapatikane kwa hii shida ya usafiri, hata wataalam wake wakaumiza kichwa, wakaja na majibu ya kubomoa kiaina, malori madogo, ya tatu tatu, ambayo mengi yao yalikuwa aina ya 'Toyota Canter', na kuwa mabasi ya abiria.

Binadamu, we acha tu, sijui huko huko Baraza la Mawaziri, au kwetu uswahilini, ule mtindo wa kukaa tu kwenye usafiri mpya uliotukomboa, picha moja kwa moja ikaangukia kama tuko kwa mama ntilie kwenye benchi letu, tukipata chai kwa maharage mapema asubuhi, labda na chapati mbili, muda ule ule ambao ndiyo tunakimbilia shughuli zetu.

Kwa staili ile ile ya wanafunzi wanapompa jina mwalimu ndani ya siku mbili tatu za ugeni wake, he kushangaa, mji mzima magari hayo yakaanza kuitwa



Wateja wanavyokaa wanapokuwa kwa mama ntilie, au mama lishe. Ukaaji huu ndiyo unafananishwa na ule wa kwenye aina ya magari ya Canter, yanaitwa 'chai maharage.'

'chai maharage', madereva wakanogewa nalo, makonda nao ndiyo usiseme, utingo ndiyo kabisa, kila kituo, wanaweka sauti ya jina hilo.

Abiria ndiyo wakabatiza kabisa, inadondoka safari kuelekea miaka 40 sasa, lakini jina bado limeendelea kuwa pale pale na hakuna dalili ya kuhama, japo kwa sasa magari hayo hayapo tena, hasa bara, ila mlo wa chai maharage umeendelea kuwa bado sehemu ya maisha, na mkao umeendelea kuwa ni ule ule, nyenzo ni zile zile hakuna mabadiliko.

Baada ya 'chai maharage', ndipo yalipokuja aina nyingine mabasi ya usafiri.

Yakaja mabasi madogo aina ya hiace.

Hii ni baada ya jitihada kubwa za Mzee Mwinyi, ambaye baada ya 'kusovu' tatizo la mwanzo la usafiri, baadaye akaona aanze kulimaliza kabisa, ndipo aina hiyo ya mabasi yakaja.

Wabongo kama kawaida yao, hawakukosa kutoa jina. Yenyewe wakayaita 'vipanya.' Sababu yake kubwa ni kuweza kupenya sehemu nyembamba ambayo kwa basi la kawaida la usafiri lisingeweza.

Jinsi lilivyotengenezwa, liliweza kuingia barabara kubwa, ndogo, hata uchochoroni bila tabu yoyote, ndipo lilipotokea jina hilo, wakiyafananisha na panya ambaye anaweza kupenya au kupita popote pale hata eneo ambalo ni dogo ambalo kwa kawaida usingedhani kama anaweza kupenya.

## Blinken awasili Israel kuomba vita kusitishwa

**TEL AVIV,** ISRAEL

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken, amewasili nchini Israel kumalizia ziara yake katika nchi za Mashariki ya kati.

Waziri Blinken, atakuwa katika kituo chake cha mwisho cha ziara yake ya sita alizofanya katika eneo hilo tangu kuanza kwa vita kati ya Israel na wanamgambo wa kundi la Hamas katika ukanda wa Gaza.

Kiongozi huyo wa ngazi ya juu wa Marekani, alisema akiwa nchini humo atapendekeza njia mbadala kuhusu mashambulizi ya ardhini yaliyopangwa kufanywa na vikosi vya Israel katika mji wa Rafah ulioko Kusini mwa Gaza.

Alisema pendekezo hilo atalitoa wakati atakapokutana na waziri mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu na baraza lake la mawaziri la vita.

Awali Blinken na viongozi wa mataifa ya kiarabu walijadili kuhusu juhudi za kusitisha mapigano na hatma ya Ukanda wa Gaza baada ya vita.

Wakati huo huo, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilitarajiwa kupiga kura jana kuhusu azimio lililowasilishwa na Marekani la kutangaza umuhimu wa kusitishwa vita mara moja.

**DW**

## Niger yatangaza maombolezo

**NIAMEY,** NIGER

SERIKALI ya kijeshi ya Niger imetangaza maombolezo ya siku tatu baada ya wanajeshi 23 kuuawa katika shambulio la kuvizia.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi wakati wa operesheni ya jeshi kati ya maeneo ya Teguey na Bankilaré, katika jimbo la Tillabéri.

Kulingana na taarifa kutoka vyombo vya habari, vilieleza wanajeshi hao walivamiwa na watu wanaodaiwa kuwa magaidi wanaofikia 100 waliokuwa kwenye magari na pikipiki, kulingana na taarifa kwa vyombo vya habari.

Shambulio hilo lilitokea katika eneo la Tillabéri, linalojulikana kuwa maficho ya wanajihadi wa Sahel, wakiwemo wale wa Islamic State na Al-Qaeda.

Wizara ya Ulinzi ilitangaza kuwa itawaheshimu wanajeshi waliouawa kwa kutoa siku hizo za maombolezo ya kitaifa.

Shambulio hilo lilitokea katika eneo ililoko katika eneo linaloitwa mipaka mitatu ambalo linapakana na nchi za Mali na Burkina Faso.

Kwa miaka mingi, sehemu hiyo ya Niger imekuwa ikilengwa mara kwa mara na mashambulio ya makundi haya yenye silaha licha ya kupelekwa kwa vikosi vya kupambana navyo.

**RFI**

# Museveni amteua mtoto wake mkuu wa majeshi

**KAMPALA,** UGANDA

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni amemteua mtoto wake wa kiume Jenerali Muhoozi Kainerugaba kuwa mkuu wa majeshi wa nchi hiyo.

Hata hivyo, uteuzi huo umeibua minong'ono huku wengi wakiamini kuwa kiongozi huyo anamsafishia njia mtoto huyo kuwa rais.

Jenerali Muhoozi Kainerugaba anachukua nafasi ya Jenerali Wilson Mbasu Mbadi ambaye ameteuliwa kuwa waziri wa biashara katika mabadiliko mapya ya baraza la mawaziri yaliyotangazwa jana jioni.

Kwa mujibu wa taarifa ya jeshi, washauri wake wawili wa karibu pia wamepewa nyadhifa za uwaziri na kuchochea uvumi kwamba Rais Museveni anaunga mkono shughuli za kisiasa za mtoto wake.

Jenerali Muhoozi Kainerugaba ambaye ni mtoto wa kwanza wa Rais Museveni amekuwa akifanya mikutano ya hadhara nchini kote, hatua ambayo inakwenda kinyume na sheria inayowazuia maofisa wa jeshi kujihusisha na siasa.

Hata hivyo, Jenerali Kainerugaba amejitetea kwa kueleza kuwa mikutano hiyo ya kisiasa ikiwa ni pamoja na uzinduzi wa kundi la uanaharakati la Patriotic League of Uganda (PLU), inanuia kuhimiza kujenga uzalendo miongoni mwa Waganda.06:34

Rais Museveni ambaye kwa mara ya kwanza alichukua madaraka kwa nguvu mnamo mwaka 1986, na kuchaguliwa mara sita katika nafasi hiyo, hajaeleza lini ataachia kiti hicho.

Kiongozi huyo hana mpinzani ndani ya chama tawala cha NRM, huku wachambuzi wa kisiasa wakiamini jeshi litakuwa na sauti katika kuchagua mrithi wake.

Kulingana na wachambuzi hao washirika wa Kainerugaba wameteuliwa kimkakati kwenye nafasi za juu za idara ya usalama.

Uganda itaandaa uchaguzi mkuu mwaka 2026.

Kiongozi wa upinzani Dk. Kizza Besigye amesema kwamba nchi hiyo kila eneo limetekwa na familia ya kiongozi huyo.

Baadhi ya watu, walieleza kuwa hatua hiyo ya Rais Museveni ni kama kutaka kumdhibiti mtoto wake ambaye alikuwa ametangaza kugombea urais na kuzindua vuguvugu la kumpigia debe.

Wiki iliyopita vuguvugu hilo liliendesha mkutano wa hadhara katika mojawapo ya ngome kuu za upinzani mjini Masaka na kuvutia umati mkubwa wa watu.

**DW**



Wakimbizi wa Rohingya waliokolewa baada ya boti yao kupinduka na kuhofia wengine wengi kufa kwa maji karibu na pwani ya kaskazini mwa Indonesia juzi. **PICHA: AP**

# Spika ajisalimisha polisi adaiwa kuomba rushwa

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

SPIKA wa bunge la Afrika Kusini, Nosiviwe Mapisa-Ngakula, amejisalimisha mikononi mwa polisi baada ya kufanyiwa uchunguzi katika kashfa ya ufisadi inayomwandama.

Mapisa-Nqakula alijisalimisha katika kituo cha Polisi ya Kati cha jijini Pretoria jana asubuhi na alitarajiwa kufikishwa mahakamani majira ya mchana. Kulingana na ripoti za vyombo vya habari, spika huyo anadaiwa kuomba rushwa ili kutoa kandarasi wakati alipokuwa waziri wa ulinzi.

Hata hivyo, haijafahamika kama polisi walimkamata na kumweka mahabusu.

Vyombo vya habari vya ndani vinaripoti kwamba Mapisa-Ngakula aliwasilisha hati za dharura ya kuzuia polisi kumlaza mahabusu.

Shirika la utangazaji la serikali la SABC, linaripoti kuwa mtuhumiwa huyo aliomba kukabidhi hati yake ya spika ili aachiwe huru. Alhamisi, Mapisa-Ngakula alitangaza kuchukua likizo maalumu na kuacha majukumu yake kutokana na uzito wa madai hayo na bunge lilimruhusu.

Mwanzoni mwa wiki, nyumba yake iliyoko Johannesburg ilivamiwa na kitengo cha polisi ambao walifanya upekuzi wa saa tano.

Hata hivyo, Spika huyo anakana madai hayo na kueleza hana hatia na kusisitiza kwamba anashirikiana na wachunguzi katika suala hilo.

**BBC.**



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Ujumbe wa Amref ukiongozwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (wa pili kushoto), walipofika Ikulu jijini Zanzibar jana, kutoa salamu za pole kutokana na kifo cha Rais mstaafu, Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi na mazungumzo. Kulia kwa Rais ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Amref, Dk. Githinji Gitahi. **PICHA: IKULU**

# Dhamana ya biashara nje kunufaisha wanawake

**Na Joseph Mwendapole**

MPANGO wa dhamana ya kuuza bidhaa nje ya nchi unaweza kuwa na manufaa makubwa kwa wafanyabiashara wanawake wanaotaka kusafirisha bidhaa kwenye masoko ya nje ya nchi.

Mkurugenzi wa Biashara ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi John Ulanga, alisema hayo hivi karibuni wakati wa utoaji wa tuzo kwa wanawake wafanyabiashara iliyoandaliwa na Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC).

Akitoa mada kuhusu nafasi ya mwanamke katika maendeleo endelevu, Balozi Ulanga alisema hakuna mafanikio yoyote yanaweza kupatikana kama kundi kubwa kwenye jamii kama wanawake wataachwa nyuma.

Mpango wa dhamana kwa wanawake wafanyabiashara, alisema ni muhimu kwani wengi wanapata masoko ya kupeleka bidhaa zao lakini wanashindwa kwa kukosa mtaji wa uhakika hivyo aliishauri TWCC kuanzisha mpango huo kuwakomboa wanawake wafanyabiashara.

"Kuna mwenzenu mmoja hapa amepata zabuni ya kupeleka mkonge Ghana lakini amekosa mtaji kama wa Sh. milioni 200. Sasa mngekuwa na mpango wa dhamana mngemkwamua akapeleka bidhaa zake bila kikwazo," alisema.

Ulanga alisema TWCC inaweza kuanzisha mpango huo kwa kushirikiana na mifuko ya serikali na taasisi mbalimbali binafsi za fedha na unaweza kuwasaidia wanawake kwa kiwango kikubwa kukuza biashara zao.

"Najua nyuma huko tuliwahi kuwa na kitu kama hiki tukakwama lakini naamini kila jambo na wakati wake na kwa wakati huu tukianzisha huu mpango tutafanikiwa tusiangalie yaliyopita tuanze upya tusonge mbele," alisema Ulanga.

Aidha, Balozi Ulanga aliishauri TWCC kuandaa ripoti ya kila mwaka inayoelezea maendeleo ya wafanyabiashara wanawake na changamoto walizokutana nazo kwenye biashara zao.

Alisema ripoti hiyo itasaidia kujua hatua ambayo wanawake wamefikia, changamoto zao na itasaidia watoa maamuzi kuweka mikakati ambayo itakikisha wafanyabiashara hao hawakwami tena kusaidia kwenye mkwamo.

Balozi Ulanga aliitaka TWCC kuendelea kufanyakazi kubwa ya kuhamasisha wanawake wengi zaidi kujingiza katika biashara na ujasiriamali ili kuondokana na umaskini

Vile vile, aliwataka wanawake wafanyabiashara kuangalia fursa za masoko mengine ya Afrika, Ulaya na Marekani badala ya kuangalia soko dogo la Tanzania pekee.

"TWCC wasaidieni wanawake hawa kuratibu namna ya kuuza nje biashara zao na mzitumie balozi zetu mnapokwama kwasababu kazi ya balozi zetu ni kuwezesha biashara kwa hiyo msiogope kuja kwenye balozi kuomba msaada," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE), Latifa Mohamed, alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa TWCC, Mwajuma Hamza, kwa namna ambavyo amekuwa mbunifu katika kusimamia kazi za chemba hiyo.

Aliwahakikisha wanawake hao wafanyabiashara kuwa fursa za masoko ya bidhaa mbalimbali za Tanzania yapo ila wanachotakiwa ni kuendelea kusimamia ubora wa bidhaa wanazozalisha.

"Mara nyingi utasikia wafanyabiashara wanalalamikia uhaba wa masoko lakini niwahakikishie masoko yapo ni sisi kuyatafuta na ili kuyafikia lazima tuwe wabunifu na tusiige vinavyofanywa na wengine tutengeneze vitu ambavyo wengine hawana," alisema.

Aliwataka wanawake wafanyabiashara kutumia mitandao ya kijamii kama fursa ya kibiashara ya kutafuta masoko maeneo mbalimbali duniani badala ya kuhangaika na mambo ambayo hayana tija kwao kibiashara.

Tuzo hizo zinazofanyika kwa mara ya nne zinafadhiliwa na Trade Mark Africa (TMA) na kupitia tuzo hizo wanawake wengi wamehamasika kuanzisha biashara zao.

## Dk. Mwinyi aipa kongole AMREF

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amelipongeza Shirika la Kimataifa linaloshughulikia masuala ya afya la AMREF kwa kufanikisha mkutano wao uliofanyika Zanzibar uliowashirikisha mawaziri wa afya kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika

Dk. Mwinyi alitoa pongezi hizo jana Ikulu, Zanzibar, alipotembelewa na uongozi wa shirika hilo ulioambatana na ujumbe wa mawaziri hao kwa lengo la kumpa pole baada ya kufiwa na baba yake mzazi, Mzee Ali Hassan Mwinyi, hivi karibuni. Mzee Mwinyi alikuwa Rais mstaafu wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais Mwinyi alisifu hatua ya mkutano huo kushirikisha mataifa mbalimbali ya Afrika na kujadiliana masuala ya afya na changamoto za afya zinazoikumba Afrika.

Alisema, AMREF ni mdau muhimu kuwahi kufanyakazi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa kwenye sekta ya afya.

Dk. Mwinyi pia alieleza ushirikiano wa karibu uliopo baina ya AMREF Tanzania na kuwa ni mzuri kwa kuwa shirika hilo limekuwa likiunga mkono juhudi za serikali kwa misaada mbalimbali, vifaa, mafunzo na kubadilisha uzoefu kwenye masuala ya afya kwa lengo la kuboresha sekta hiyo.

Aidha, Rais Mwinyi aliushukuru ujumbe huo kwa kumfariji kutokana na kufiwa na baba yake mzazi hivi karibuni.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa AMREF Health Africa Group, Dk. Githinji Gitahi, alimwelea Rais Dk. Mwinyi azma ya kuwapo kwao Zanzibar baada ya kufanikisha mkutano wa kimataifa wa mawaziri wa afya kutoka Afrika ambao walijadili na kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha sekta ya afya Afrika pamoja na kudhibiti magonjwa mbalimbali yakiwamo malaria na yale yasiyo ya kuambukiza.

Wakati huo huo, Mkurugenzi wa AMREF - Tanzania, Dk. Florence Temu, alimweleza Rais Mwinyi kwamba shirika hilo limekuwa na ushirikiano wa karibu na serikali za Zanzibar na Muungano.


KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA YA KINONDONI
MWANANYAMALA

SHAURI LA MADAI NAMBARI 73 LA 2024

EUNICE M. KIHAMIA.................MOUMBAJI/WAOMBAJI

DHIDI YA

ROZY C. KIHAMIA..................MDAIWA/WADAIWA

WITO KUITWA SHAURINI

ROZY C. KIHAMIA – POPOTE ULIPO/MLIPO

**EUNICE M. KIHAMIA** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 26/3/2024 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 18 Mwezi 03, 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI



**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**GALLISS ROBERT MAKUNJA** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE370969** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 12/11/2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/61320/2024.**



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**HASSAN KOMBO MAKATA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 455 ASD.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/TAN/1357/2024.**



**KUPOTEA KWA OFFER YA KIWANJA**

**JUMANNE RAMADHANI SALUMU** anatangaza kupotea kwa **OFFER YA KIWANJA** cha Marehemu Baba yake **PLOT NO. 128, BLOCK A CHAMWINO – DODOMA CITY COUNCIL.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/8362/2024.**



THE REGISTRATION OF DOCUMENT ACT,
[CAP.117 R.E.2002
CHANGE OF NAME BY DEED POLL

**BY THIS DEED POLL**
**I, SIYELA RASHIDI KASENDEKA** an adult, Muslim, a resident of Shede Street within Kigoma Ujiji Municipality with mobile No.0756086855 do hereby solemnly declare to denounce and abandon the use of my first name **"SIYEVELA"** in my names of **"SIYEVELA R.KASENDEKA** where by letter "R" stands for RASHIDI. Hence in lieu thereof do assume from the date of registration thereof the name of **SIYELA RASHIDI KASENDEKA** as my true name.
And in pursuance of such abandon of the said first name **"SIYEVELA"** in my names of **"SIYEVELA R. KASENDEKA"** I hereby declare that at all time hereinafter in all records, deeds, documents instruments in writing, in all actions proceedings as well as in all public and private dealings and transactions and in all occasions whatsoever use and subscribe me as **"SIYELA RASHIDI. KASENDEKA"** accordingly.
And I hereby authorize and request all persons whomsoever, at all time after the date of presents to designate, describe and address me by the adopted name of **SIYELA RASHID KASENDEKA** accordingly.
The reasons for denounce and abandon the said first name **"SIYEVELA"** is af follows:
The said first name of **"SIYEVELA"** in my names of **"SIYEVELA R. KASENDEKA"** was wrongly written in my payment letter from PPF currently known as Public Social Services Security Fund (PSSF) dated 6th day of September, 2007. Hence I adopted to use the first name of **SIYELA"** in my names **SIYELA RASHIDI KASENDEKA** as it appears to my Citizen Identity Card with No. 19641212-47101-00003-26.

**I, SIYELA RASHIDI KASENDEKA** declare that all what is stated herein above is true to the best of my knowledge and in accordance with the provisions of Registration of Documents Act Cap 117 and *Oaths and Statutory Declarations Act, Cap 34 R.E. 2019.*
**IN WITNESS WHEREOF,** I have executed this deed this 18 day of March 2024

DEPONENT

**SIGNED** and **DELIVERED** by the said **SIYELA RASHIDI KASENDEKA** who is known to me personally this 18 day of March 2024

DEPONENT



**BEFORE ME:-**
Name: **SILVESTER DAMAS SOGOMBA**
Signature......................
Qualification: Commissioner for oaths
Address: P.O Box 797 KIGOMA

**DRAWN BY:-**
Silvester Damas Sogomba (Advocate),
P. O. Box 797,
**KIGOMA.** (0764154859)

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-**5**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.

Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.

Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.

Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani.

Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

Alipogeuka kumuangalia akamwambia. "Chukua huyo mkubwa kuliko wote hapo, nimeamua kukuchagulia."

"Mmmh! Mkubwa huyu bei yake nitaiweza?"

"Nimekwambia chukua, bei yake nitaiweza mimi!" Akajibu Kamal na Mariamu alimuelewa.

Baada ya kumchukua samaki yule mkubwa, Kamal naye akachagua yule ambaye alitaka kumnunua Mariamu. Kwenye mkoba wake Mariamu alikuwa na sahani ya karatasi, akazitoa mbili na kumpa moja Kamal naye awekee samaki wake.

Muuza mihogo ya kuchemsha naye akapita wakanunua minne, kila mmoja akachukua miwili. Pesa zote alilipa Kamal.

"Haya sasa tule, mimi nakula samaki niliokuchangulia na mimi nakula huyu uliomchagua wewe." Kamal aliposema maneno hayo, Mariamu akamtazama kwa macho ya kumuiba mara moja na kuyaondoa, akatabasamu.

Akatoa khanga yake akatandika kwenye nyasi, wakakaa na kuanza kula. Lilikuwa ni kosa kubwa kwa Mariamu kumpa nafasi ya kuongea na kujitetea. Kesi ikawa imeishia hapo.

Walikaa na kula. Wakaongea mengi. Ilionekana kama kila mtu alikakwepa kuongea kilichotokea ndani ya basi. Ni kwa sababu walipatana. Kiasi Mariamu alianza kuona alikosea jinsi alivyomtazama kijana huyo mwanzo.




Kwa muda mfupi tu, aligudua kuwa ni kijana mwerevu, mcheshi, mwenye upendo na siyo kama kile alichokiona ndani ya basi.

Akaanza kuamini kuwa alikuwa anaigiza. Akaamini alifanya hivyo kwa ajili ya kulinda uanaume wake ndani ya basi, asionekane bwege. Ndiyo akaamini hivyo.

"Tumejitahidi sana, tumekula bila maji, na hii mihogo du!" Kamal akavunja ukimya uliotawala kwa muda.

"We acha tu!" Mariamu akajibu.

"Hasa nilikuwa nakuonea huruma wewe, mimi nimeshazoea."

"Waswahili wanasema msafiri kakiri, tuko safarini huwezi ukajiachia kama uko nyumbani, kuna vitu vingine lazima nikupite, ujibane, siyo ujiachie kama uko nyumbani."

Walipomaliza walisimama, Mariamu akachukua khanga yake aliyotandika chini, akaikung'uta na kuirudisha kwenye mkoba wake.

"Twende pale kidogo, wakati napita nimeona kuna kiduka hivi, tukanunue maji, maana tumekula kama nyoka."

Mariamu akakubaliana na Kamal, wakaanza kutembea hatua za taratibu kuelekea wanakokwenda.

Abiria wachache waliowaona walishtuka na kushangaa kwa wakati mmoja. Abiria wenzao wawili waliokuwa wakigombanisha siti ya dirishani wamepatana!

Kwa jinsi hali iliyoonekana ndani ya basi, hawakutegemea kwa kipindi hiki wakiwa wamekaa pale bibie akiwa ametandika khanga wanakula, halafu wamenyanyuka na kuongozana kama kumbikumbi.

Walirejea kila mmoja akiwa ameshika chupa kubwa ya maji ya Kilimanjaro mkononi.

Dereva alipiga stata na basi likawaka ikiashiria tayari mafundi wameshafanikiwa kutengeneza baada ya kuweka kifaa kilichoagizwa kutoka Morogoro mjini, tayari kuendelea na safari ya kuelekea Dar es Salaam.

Konda yule yule aliwataarifu abiria wote wapande kwenye basi, tayari kwa safari. Ilipohakikishwa kuwa hakuna abiria yoyote aliyeachwa, basi liliondoka.

Abiria alishuhudia kitu cha ajabu. yule mwanada mrembo aliyekataliwa kukaa siti ya dirishani na abiria mwenzake wa kiume, sasa amekaa tena kwa tabasamu na bashasha.

Kuna wale alioona mchezo umebadilika kule nje wakati basi linatengenezwa.Wengi walikuwa hawajaona kwa sababu waliingia mitaani ili kupoteza muda. Hao ndiyo walioshangaa zaidi.

Mshangao uliwazidi pale walipoona yule kijana waliyemtoa kwenye siti ya dirishani kwa sababu alikuwa amekaa yeye kabla, amekaa hapo hapo pembeni yake, wakizungumza kama hapakuwa chochote kabla yao.

**Kwa jinsi hali iliyoonekana ndani ya basi, hawakutegemea kwa kipindi hiki wakiwa wamekaa pale bibie akiwa ametandika khanga wanakula, halafu wamenyanyuka na kuongozana kama kumbikumbi.**

"He! wamepatana hawa?" Abiria mmoja akajiuliza. "Mhh! Wamepatana vipi hawa?" Mwingine akajuliza. Mwingine akajiongeza kwa kumpongeza kijana kimoyomoyo "Kijana huyu atakuwa na uwezo mkubwa wa kushawishi. Kwa hali ile, hakuna mwanamke yoyote ambaye angekubali kuongea naye, achilia mbali kukubali tena kukaa dirishani.

"Kwa urembo aliokuwa nao dada huyu, inaelekea jamaa alikuwa anajibaraguza tu. Hata mimi ningemuomba msamaha baadaye." Huyu alikuwa karibu na ukweli.

Kamal ndivyo alivyoamua. Alipopanda na Mariamu, akamwambia. "Wewe sasa kaa dirishani."

"Wewe je?" Akauliza Mariamu. "Nitakaa baadaye. Nilikwambia nilichofanya hakikuwa kitu halisi. Nilifanya kwa makusudi na kwa sababu maalum ambayo nimekueleza. Mpamgo umeshafaulu." Akamnong'oneza.

Ndani ya basi pamoja na kwamba Kamal na Mariamu walikuwa gumzo, walikuwa pia kivutio, kwani mara kwa mara walikuwa wanabadilishana kukaa dirishani hadi basi lilipofika Stendi ya Basi ya Magufuli.

"He! Yaani tumekuwa wote tunaongea tangu Bwawani, lakini nilikuwa bado sijakuuliza jina hadi tunafika!" Mariamu akaangua kicheko, halafu akamwambia. "Yaani unaongea na mtu humjui jina?" "Naye akauliza kiutani akiendelea kucheka."

Walikuwa ndiyo kwanza wanateremka kwenye basi, halafu ilionekana kama wanaelekea sehemu moja wakati sivyo.

Abiria wote ndani ya basi hilo wakaamini ule msemo wa 'wagombanao ndiyo wapatanao.' Kwa sababu walishuhudia kwa macho yao, watu wawili wakigombana ndani ya basi wakati linaondoka Stendi ya Basi Msamvu, Morogoro, lakini wanateremka wakiwa pamoja, wakiongea kwa bashasha kwenye Stendi ya Mabasi ya Magufuli.

"Kwani na wewe unanijua jina?" Kamal akamuuliza.

"Mhh! Sikujui kwa kweli."

"Sasa kwa nini unanicheka mimi kutojua jina lako. Mimi naitwa Kamal."

"Mimi naitwa Mariamu."

"Okay, jina zuri kama wewe mwenyewe!"

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KATOLIKI JIMBO LA DAR WAANDAA MARATHON

Na Mwandishi Wetu

KANISA Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam limeandaa mashindano ya riadha ya nusu marathon yatakayohusisha zaidi ya watu 10,000 huku wakiwa na lengo la kukusanya fedha kuwasaidia watu wenye mahitaji mbalimbali katika jamii.

Mashindano hayo ya mwaka huu yamepangwa kufanyika Mei 18 kwenye viwanja vya Hija, Pugu jijini Dar es Salaam.

Mbio hizo kwa mwaka huu zitashirikisha kukimbia kuanzia umbali wa Kilometa mbili, Kilometa tano, Kilometa 10 na Kilometa 21 kwa watu mbalimbali.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Askofu Mkuu wa jimbo hilo, Yuda Thedeues Ruwa'ichi, alisema mbio hizo kwa mwaka jana zilikuwa na mafanikio makubwa na wanaamini mwaka huu zitakuwa na mafanikio zaidi.**

"Napenda kuwataarifu watu wote kuwa mbio za mwaka huu zitafanyika Mei 18, nawakaribisha watu wote kushiriki ili kufikia malengo yetu ya kuwasaidia watu wenye uhitaji katika jamii zetu," alisema Askofu Ruwa'ichi.

Aidha, alisema mbio za mwaka jana walifanikiwa kukusanya shilingi milioni 117 ambazo walizitumia kutoa misaada kwenye vituo vya watoto yatima, kununua mashuka 100 kwenye hospitali ya Kardinali Rugambwa na mwaka huu wanatarajia kuvuka hapo.

"Siku ya mbio kutakuwa na shughuli mbalimbali, kutakuwa na zoezi la kupima afya, kuchangia damu, kujenga imani ya kanisa na mambo mengine mengi," alisema Ruwa'ichi.

Alisema kwa mwaka huu mbali na kusaidia watu wenye mahitaji kwenye jamii pia wamepanga kuboresha maktaba kwenye shule ya Sekondari ya Pugu kwa kuanzisha maktaba ya mwalimu Julius Nyerere.

Mbio hizo zinatarajiwa kuanza saa 12 asubuhi ambapo makundi yote kama Mapadre, Watawa, Wawata, Viwawa watashiriki.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Luchelele ya jijini Mwanza wakicheza mpira maarufu kama 'sembo' wakati wa mapumziko shuleni hapo. **PICHA: VITUS AUDAX**

# *Uchaguzi makocha wa riadha Machi 24*

Na Shufaa Lyimo

UCHAGUZI wa Chama cha Makocha wa Riadha Tanzania umepangwa kufanyika Machi 24, mwaka huu jijini, Dodoma.

Ofisa Uhusiano na Mawasiliano wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Najaha Bakari, amewataka wadau kujitokeza kuchukua fomu na kuwania nafasi mbalimbali za uongozi wa chama hicho.

Najaha alisema fomu zinatolewa katika ofisi za baraza hilo na kuzitaja nafasi zinazowaniwa ni pamoja na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Katibu Msaidizi, Mweka Hazina na Wajumbe wanne wa Kamati ya Utendaji.

"Mpaka sasa mwitikio sio mzuri, tunaomba wagombea waje kuchukua fomu kwa sababu siku zimebaki chache, tunataka kila chama kifanye uchaguzi ili kupata viongozi watakaoleta mabadiliko," alisema Najaha.

Aliongeza kwa kuwasisitiza wadau wote wenye vigezo kwenda kuchukua fomu ili kugombea na hatimaye chama kupata viongozi watakaokiongoza kwa weledi.

## Vyama vyatakiwa kulipa ya serikalini

Na Shufaa Lyimo

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limetoa siku saba kwa vyama na mashirikisho ya michezo nchini kulipa malimbikizo ya ada wanazodaiwa kabla ya kuchukuliwa hatua, imeelezwa.

Msajili wa Vyama vya Michezo wa (BMT), Evordy Kyando, aliliambia gazeti hili jana chama ambacho hakitakuwa kimelipa ada wanazodaiwa katika muda huo waliopewa watatozwa faini ya asilimia tano ya deni lake.

"Baada ya siku saba kama kutakuwa na chama au shirikisho ambalo halijalipa ada yake ya mwaka kitatozwa faini ya asilimia tano, tunawakumbusha kulipa ada kwa sababu fedha hizi zinasaidia katika majukumu ya kuendeleza michezo hapa nchini," alisema Kyando.

Alisema kwa upande wa vyama vya mpira wa miguu 28 vilivyosajiliwa, mpaka sasa hakuna ambacho kimelipa ada hiyo inayotambulika kwa mujibu wa sheria.

"Wiki ijayo ninatarajia kuwataja hadharani wadaiwa sugu ili kila mtu awafahamu, sitalifumbia macho suala hili kwa sababu wa baadhi ya watu wanafanya masihara," Kyando aliongeza.



**Wiki ijayo ninatarajia kuwataja hadharani wadaiwa sugu ili kila mtu awafahamu, sitalifumbia macho suala hili kwa sababu ya baadhi ya watu wanafanya masihara.**
Evordy Kyando

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

## GOMES ALENGWA UNITED

KLABU ya Manchester United inamlenga kiungo wa Wolves, Joao Gomes, 23, kuwa mbadala wa Mbrazil mwenzake, Casemiro, 32. ***(Mirror)***

## RODRYOGO AWINDWA

ARSENAL, Liverpool, Manchester City na Manchester United zote zinamtaka mshambuliaji wa Real Madrid, Rodrygo, 23, na miamba hao wa Hispania wanaweza kushawishiwa kufanya mazungumzo iwapo watapokea ofa ya pauni milioni 85. ***(Sport)***

## MATIP KURUHUSIWA

LIVERPOOL inapanga kumruhusu mlinzi wa zamani wa Cameroon, Joel Matip mwenye umri wa miaka 32, kiungo wa zamani wa Hispania, Thiago Alcantara, 32, na mlinda lango wa Hispania, Adrian, 37, kuondoka msimu huu wa joto. ***(Football Insider)***

## GREENWOOD HAKIELEWEKI

MATUMAINI ya klabu ya Getafe ya kumsajili tena kwa mkopo mshambuliaji wa England, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22 msimu ujao yanatazamiwa kukatizwa huku Manchester United wakihitaji mkataba wa kudumu iwapo wataamua kumwacha. ***(Sun)***

## BARCELONA NA ONANA

BARCELONA ipo tayari kuwapa Everton chaguo la wachezaji wanne, winga wa Hispania, Ansu Fati mwenye miaka 28, mlinzi wa kati wa Ufaransa, Clement Lenglet mwenye miaka 23, mlinzi wa kulia wa Marekani, Sergino Dest mwenye miaka 20 na kiungo wa zamani wa Hispania, Fermin Lopez. Hiyo ni kwa ajili ya wao kumpata kiungo wao wa kati wa Senegal aliyekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 80, Amadou Onana mwenye miaka 22. ***(Sport via Teamtalk)***

## KOOPMEINERS KUONDOKA

KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Teun Koopmeiners ameiambia klabu yake ya Italia, Atalanta kuwa anataka kuondoka msimu huu wa joto, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 akihusishwa kuelekea Liverpool. ***(Metro)***

## HAG BADO SANA

KAZI ya kocha wa Manchester United, Erik ten Hag iko salama kwa msimu uliobakia baada ya kumvutia Sir Jim Ratcliffe katika hatua za awali za wakati wa mmiliki mwenza mpya katika klabu hiyo. ***(Guardian)***

## WERNER NA MKATABA

MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 28, anataka kubadilisha mkopo wake kutoka RB Leipzig hadi Tottenham Hotspur kuwa uhamisho wa kudumu ambao unaweza kuigharimu klabu hiyo chini ya pauni milioni 15. ***(Telegraph)***

## SOUTHGATE NA ENGLAND

MSHINDI mara saba wa Ligi Kuu ya England akiwa na Manchester United, Roy Keane amesema "niliona hilo likifanyika" alipoulizwa kuhusu klabu hiyo kuhusishwa na kocha wa England, Gareth Southgate. ***(Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SAKA AZUSHA HOFU

### Ni baada ya kujiondoa kwenye kikosi cha timu ya taifa cha England kutokana na...

**LONDON,** England

WINGA wa Arsenal, Bukayo Saka amejiondoa kwenye kikosi cha England kabla ya mchezo wa leo Jumamosi wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Brazil na ule wa Jumanne dhidi ya Ubelgiji kutokana na majeraha.

**Saka alikuwa majeruhi tangu alipowasili kwenye kikosi cha England na sasa hatakuwa sehemu ya mechi za timu hiyo.**

Taarifa kutoka timu ya England ilisomeka: "Bukayo Saka ameondoka kwenye kambi ya England na amerudi kwenye Klabu yake kuendelea na matibabu. Fowadi huyo wa Arsenal aliwasili kwenye kambi pale St. George's Park akiwa majeruhi na hivyo alishindwa kushiriki kwenye mazoezi.

"Hakuna mchezaji aliyepangwa kuchukua nafasi katika kikosi hicho cha wachezaji 25 kwani wanaendelea na maandalizi yao ya mechi za kimataifa dhidi ya Brazil na Ubelgiji."

Kukosekana kwa Saka kwenye kikosi cha England hakuna shaka kubwa licha ya kukatisha tamaa kuelekea mandalizi ya Euro 2024, lakini anaonekana kutokuwa na majeraha makubwa.

Hata hivyo, amezusha hofu ya kuwa fiti kabla ya mchezo wa Ligi Kuu England wa Arsenal dhidi ya Manchester City wakati ligi zitakaporudi mwishoni mwa mwezi huu.

Gabriel Martinelli na Gabriel Magalhaes pia hawapo kwenye kikosi cha Brazil kutokana na majeraha na pia wanatia shaka uwezekano wa kuwepo kwenye mchezo dhidi ya City hadi hapo taarifa zaidi zitakapotolewa.

Litakuwa pigo kubwa kama Saka atakosa safari ya kwenda kwenye dimba la Etihad kama hatapona kwa wakati.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ndie mfungaji anayeongoza kwa ufungaji magoli katika kikosi cha Arsenal msimu huu, akifunga mabao 16 katika mashindano yote.

Ana asisti 13 na kumfanya kuwa jumla na mchango wa mabao 29 katika mechi 37 za Klabu yake.

# GREALISH KUPIGWA BEI MAN CITY



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City huenda ikamuachia winga wao Jack Grealish katika dirisha lijalo la majira ya joto kwa ajili ya kupata fedha zitakazotumika kufanya usajili wa wachezaji inaowahitaji.

Grealish amekuwa hapati nafasi ya kutosha kwenye kikosi cha kwanza cha Man City. Mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika mwaka 2027.

Staa huyo mwenye umri wa miaka 28 hajaonesha kiwango kilichotarajiwa tangu kuanza kwa msimu huu na kocha wa Man City, Pep Guardiola, alishawahi kutamka wazi kwamba haridhishwi na kiwango chake.

Kuna ripoti zinazoeleza kuwa Man City inataka kumsajili winga wa Napoli, Khvicha Kvaratskhelia katika dirisha lijalo, ili akachukue nafasi ya Grealish.

Tangu dirisha lililopita kumekuwa na taarifa zinazomhusisha Grealish na Arsenal inayodaiwa kuandaa zaidi ya pauni milioni 50 kwa ajili ya kufanikisha mchakato wa kumsajili.

Pep anawania taji la Ligi Kuu England analolishikilia na amekuwa akitumia wachezaji wanaompa matokeo, kwani vita ya ubingwa ni kali mbele ya Arsenal na Liverpool.

Grealish amekuwa akianzia benchi au kutokucheza na hii inachangia kutaka kuondoka.

# Bayern, Liverpool mbio moja kwa Alonso



**MUNICH,** Ujerumani

RAIS wa heshima wa Bayern Munich, Uli Hoeness amesema klabu hiyo ya Bavaria inashindana na Liverpool kuwania saini ya Xabi Alonso huku zote mbili zikitarajia kuteua makocha wapya msimu huu wa joto.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp ametangaza kuachana na timu ya Merseyside mwishoni mwa msimu huu baada ya kuiongoza kwa takriban miaka tisa, huku Thomas Tuchel wa Bayern akikubali kuwaacha mabingwa hao watetezi wa ligi kuu ya Ujerumani msimu huu utakapomalizika kutokana na mwenendo mbaya wa timu.

Alonso, ambaye alizichezea klabu zote mbili anaonekana kuwa tayari kuiongoza Bayer Leverkusen kutwaa taji lao la Bundesliga kwani wanaongoza kwa pointi 10 dhidi ya Bayern wakiwa wamesalia na mechi nane.

"Klabu kama Liverpool, Real Madrid, Leverkusen na FC Bayern zinashughulikia kumuajiri Alonso," alisema Hoeness akiambia kituo cha Ujerumani cha Ran.

"Amethibitika kuwa anaweza kuwa kocha kwa muda mrefu. Hakuna makocha wanaokuja kuhojiwa ambao kwa sasa wako huru, hawana kazi au wanaopumzika.

"Sio rahisi sana kuwaambia kwamba FC Bayern ndio kipimo cha mambo yote."

Alonso ana mkataba na Leverkusen hadi 2026 na amekataa kuhojiwa kuhusu mustakabali wake. Ameiongoza klabu hiyo kwa mbio zisizo na kifani za michezo 38 bila kushindwa katika mashindano yote.

Leverkusen imebakia kwenye kinyang'anyiro cha kutwaa mataji matatu ya kihistoria msimu huu baada ya kutinga robo fainali ya Ligi ya Europa na nusu fainali ya Kombe la Ujerumani.

# Onana kubadilishwa na wachezaji

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wamepigiwa upatu kutoa wachezaji kwa Everton huku wakitafuta kupunguza gharama ya uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati, Amadou Onana.

Onana ameng'ara katika timu inayohangaika ya Everton tangu alipowasili kutoka Lille majira ya joto ya 2022.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal, ambaye ana umri wa miaka 22, amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa, zikiwemo Arsenal, Chelsea na Manchester United pamoja na Barca. Kwa mujibu wa Sport, bei ya pauni milioni 51.5 ni tatizo lisiloshangaza kwa miamba hao wa Katalunya.

Hata pauni milioni 34 ikiwa Everton itashushwa daraja kutoka Ligi Kuu England bado itakuwa ngumu kuimudu.

Kipaumbele cha Everton, iliyoporwa pointi na kushtakiwa kwa mara ya pili kwa kukiuka sheria za kifedha, ni fedha taslimu. Lakini Barcelona wanatarajiwa kutoa wachezaji kutaka kuwa sehemu ya mabadilishano.

Lakini haitakuwa nyota wakuu au wale wanaoaminika kuwa muhimu kwa mradi wao pale Camp Nou, badala ya wale ambao wamefikia mwisho wa safari, lakini bado wana thamani - kama Clement Lenglet, Sergino Dest, Ansu Fati na Fermin Lopez.

Lenglet, Dest na Fati wako nje kwa mkopo msimu huu katika klabu za Aston Villa, PSV Eindhoven na Brighton. Wakati huo huo, Lopez anasemekana kuwa na kila nia ya kubakia Barcelona.

Mapema wiki hii, ripoti kutoka Hispania ilidokeza kwamba Onana ni mmoja kati ya majina manne kwenye orodha ya wachezaji wanaosakwa na Barcelona ili kuimarisha safu ya kiungo.



# Baridi kali yaigharimu Taifa Stars

ustadi na beki wa kati Aleks Petkov.

Allarakhia, kwa mara nyingine tena dakika ya 42 akiwa upande ule ule wa kushoto aliwalamba chenga mabeki wawili wa Bulgaria na kupiga krosi safi lakini mabeki wa Bulgaria walikuwa imara kuuondoa mpira huo kabla haujaleta madhara.

Dakika chache kabla ya mapumziko, Kawawa alifanya kazi ya ziada kwa kuokoa kiufundi mpira wa kichwa uliopigwa na Martin Minchev na kuwa kona tasa.

Stars ilipoteza nafasi tena kipindi cha pili ambapo umakini mdogo wa Feisal Salum uliwanyima goli.

Kabla mwamuzi hajapuliza filimbi ya mwisho, nusura Clement Mzize aliyeingia kipindi cha pili aisawazishie Stars baada ya shuti lake kugonga mwamba wa juu na kuokolewa na mabeki wa Bulgaria.

Kocha Mkuu Hemed Suleiman 'Morocco' katikati ya kipindi cha pili alifanya mabadiliko ya kuwatoa wachezaji watano, ambao ni Himid Mao, Kibu, Mnoga, Allarakhia na Miano Danilo, na kuwaingiza Mudathir Yahaya, Abdul Selemani 'Sopu', Lusajo Mwaikenda, Mzize na Charles M'Mombwa.

Mabadiliko hayo kwa kiasi kikubwa yaliisaidia Stars ambao walibadilika na kuonyesha soka la hali ya juu, huku ikifanya mashambulizi mfululizo na kulazimu idadi kubwa ya wachezaji wa Bulgaria kurudi nyuma.

# GAMONDI: HATUTOBADILISHA MFUMO WETU KWA MAMELODI

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi amesema licha ya umuhimu wa mchezo na ugumu wa wapinzani wao hawatarajii kubadili aina ya uchezaji kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelod Sundowns.

Yanga itakuwa mwenyeji wa Mamelodi Jumamosi ijayo kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa kutafuta nafasi ya kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo mikubwa kabisa Afrika kwa ngazi ya vilabu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Gamondi, amesema kuwa itakuwa ni hatari kwao kuhama kwenda katika mfumo mwingine wa uchezaji ambao wachezaji hawajauzoea, hiyo inaweza kupelekea kufanya makosa mengi na kuadhibiwa.

> **"Hatutabadili aina ya uchezaji wetu, tutabaki na falsafa yetu ile ile ya kutandaza soka safi, kushambulia na kukaba kwa pamoja na si kuhamahama kwa ajili ya kumuogopa mpinzani," alisema Gamondi.**

Gamondi, alisema wanawaheshimu wapinzani wao na anaifahamu vizuri timu hiyo kwa sababu amewahi kufundisha soka Afrika Kusini, kikubwa anajipanga vizuri kuhakikisha watacheza mchezo huo kwa tahadhari bila kubadili aina yao ya uchezaji.

Alisema amekua akifuatilia baadhi ya mechi za wapinzani wao na kuona ubora na madhaifu yao ambavyo vyote wanavifanyia kazi kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ya nyumbani.

"Tunatakiwa kucheza mpira wetu tuliouzoea hatupaswi kuwahofia Mamelodi Sundowns, ukihama falsafa yako utakuwa umejimaliza mwenyewe, mimi sitaki kufanya hivyo, falsafa yangu ni kucheza mchezo mzuri kumiliki na kujaribu kutengeneza nafasi, tunamuheshimu mpinzani wetu kwa kuwa wana wachezaji wazuri na wenye thamani kubwa, huu ni mpira wa miguu ukijiandaa vizuri unapata matokeo," alisema Miguel.

Aliongeza kuwa wanaendelea kujiandaa na mechi hiyo na anaimani kila mchezaji anatambua umuhimu wa kufanya vizuri katika mchezo huo wa nyumbani kabla ya kurudiana ugenini.

Alieleza kuwa amekuwa akiongea na wachezaji wake suala la kupambana na kujitoa katika mchezo huo kwa sababu ni mechi ambayo wanahitaji kutafuta ushindi na kutoruhusu bao ili mechi ya marudiano ugenini wasiwe na mlima mrefu.




Kikundi cha ngoma za asili kikitumbuiza wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la kiwanda cha kutengeneza mabati ya rangi cha Alaf jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Benchika apambana utimamu wa mwili kwa wachezaji wake*

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba kwa sasa kipo Zanzibar kikijiandaa na mchezo wao dhidi ya Al Ahly ya Misri wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku kocha Abdelhak Benchikha akiweka wazi ameanza kwa kuwajengea utimamu wa mwili nyota wake hao.

Simba imeweka kambi visiwani humo kujiandaa na mchezo huo utakaochezwa Machi 29 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.



Akizungumza jana na Nipashe, Benchikha, amesema kuwa wanahitaji kuwa imara kimwili na kiakili kuelekea kwenye mchezo huo muhimu.

Alisema watatumia kambi hiyo ya Zanzibar kuwarudishia wachezaji wake utimamu wa mwili na kuwaongezea kasi kwa sababu mchezo dhidi ya waarabu hao hautakuwa mwepesi.

"Kambi hii tutaitumia kufanyia kazi mapungufu yote niliyoyaona, moja wapo ni hili la baadhi ya wachezaji utokuwa na utimamu wa mwili, kushindwa kucheza kwa kasi ile ile kwa dakika zote, tunatakiwa kuwa fiti kabla ya kukutana na Al Ahly," alisema Benchikha.

Alisema Al Ahly wanatumia nguvu na spidi hivyo lazima wawe kamili katika idara zote kuweza kukabiliana nao na kuwatupa nje ya mashindano hayo.

Benchikha, amewaondoa hofu mashabiki wa timu hiyo kwa kile anachokifanya kwenye kambi ya timu hiyo kwa sababu tayari mabadiliko yameanza kuonekana.

"Kila mchezaji yuko vizuri na fiziki yao inazidi kupanda kila siku, nina uhakika mpaka kufika siku ya mechi utimamu wa mwili kwa wachezaji wetu utakuwa asilimia 100, na hata wale ambao wapo kwenye timu ya taifa nafahamu wanapata kitu kutoka benchi la ufundi la timu hiyo," alisema Benchikha.

# Bosi waamuzi aunga mkono

INATOKA UKURASA 24

kati ya nyenzo zitakazotusaidia sana kwenye uamuzi na waamuzi wetu kufanya maamuzi sahihi pale ambapo hawakuliona vizuri tukio ambapo kwa sasa hawawezi kufanya hivyo," alisema Hamdoun.

Hivi karibuni, TFF, pamoja na kukubali kuipokea timu ya Al Hilal ya Sudan, ilikiri pia kupokea waamuzi ambao mpango ni kutaka wachezeshe soka nchini kwenye michezo mbalimbali, ikiwemo Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Tukumbuke mahusiano kutoka nje ni moja ya jambo bora katika kuwaendeleza waamuzi wetu, kumekuwa na taarifa ambazo zimeshatolewa ufafanuzi na TFF kwamba kuna waamuzi kutoka nje ya nchi wapo hapa na wenyewe watajumuishwa kwenye ligi yetu, nawahakikishia wadau na wao wenyewe kuwa tutakuwa nao, niwaombe waamuzi wenzangu wasione kama vile wanaingiliwa, hapana.

Hii ni changamoto ni lazima wakubaline nayo, tushirikiane nao kwa namna ya kuwaongezea wao kitu na sisi pia kupata kitu kutoka kwao, wote tujifunze, tunaunga mkono hilo," alisema Bosi huyo wa Waamuzi.

# Michezo

Jumamosi Machi 23, 2024

Nipashe




Saka azusha hofu Arsenal UKURASA 21



Mshambuliaji wa timu ya taifa 'Taifa Stars', Kibu Denis (jezi ya bluu) akiwatoka mabeki wa timu ya taifa ya Bulgaria kwenye mchezo wa michuano maalum ya FIFA 'FIFA Series 2024' uliochezwa jana kwenye uwanja wa Dalga katika mji wa Baku nchini Azerbaijan. Stars ilifungwa bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Baridi yaigharimu Stars

## ●●● Yakubali kipigo cha kwanza 'FIFA Series', Kocha asema...

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU kocha wa timu ya taifa 'Taifa Stars' Hemed Suleiman 'Morocco', amesema hali ya hewa ya baridi kali imewagharimu wachezaji wake licha ya kupambana kwenye mchezo wao wa jana wa michuano maalum ya FIFA 'FIFA Series 2024' dhidi ya Bulgaria ambao walipoteza kwa bao 1-0.

**Morocco alisema tangu wamewasili kwenye mji wa Baku nchini Azerbaijan, wamekutana na hali ya baridi kali ukilinganisha na miji mingi ya Tanzania.**

Hata hivyo alisema walipambana na kucheza vizuri kwenye mchezo wa jana licha ya kupoteza mchezo huo.

"Tunaamini mchezo unaofuata tutakuwa kwenye hali nzuri na tutakuwa tumeizoea hii hali, nawapongeza wachezaji wangu kwa kucheza vizuri na kupambana," alisema Morocco.

Mchezo unaofuata, Stars itaumana na Mongolia ikiwa ni mfululizo wa michuano hiyo maalum ya mechi za kirafiki za FIFA.

Katika mchezo wa jana, bao pekee la nahodha wa Bulgaria Kiril Despodov, lilitosha kuipa ushindi timu yake.

Despodov, anayecheza pamoja na nahodha wa Stars, Mbwana Samatta kwenye klabu ya PAOK nchini Ubelgiji, alifunga bao hilo kwa mpira wa adhabu ndogo dakika ya 58, baada ya mmoja wa wachezaji wao kufanyiwa madhambi na beki wa Stars, Bakari Mwamnyeto, nje kidogo ya eneo la hatari.

Despodov alipiga faulo hiyo kifundi iliyokwenda kugonga mwamba wa juu kabla ya kuingia nyavuni upande wa kulia wa golikipa Kwesi Kawawa, aliyeingia dakika ya 30 kuchukua nafasi ya Aishi Manula ambaye alishindwa kuendelea na mchezo baada ya kuumia.

Licha ya kufungwa, wachezaji wa Stars kama wangekuwa makini wangeweza kuondoka na ushindi baada ya kuonyesha kandanda la hali ya juu, hasa kipindi cha pili lakini walipoteza nafasi za kufunga.

Dakika 20 ya mchezo, Kibu Denis alikaribia kuipatia Stars bao lakini shuti lake liligonga nguzo ya pembeni, akiwa amebaki na kipa Dimitar Mitov.

Manula alifanya kazi ya ziada dakika ya 28, alipolazimika kudaka mara mbili mpira wa kichwa uliounganishwa na Georgie Rusev, baada ya kona iliyopigwa na Valentin Antov.

Akiwa hatua tatu tu kutoka kwa aliyepiga kichwa cha juu, Manula aliruka na kuudaka mpira ambao ulimponyoka kabla ya kuudaka tena wakati akikaribiwa na wachezaji wa Bulgaria.

Msukosuko huo ulimsababishia maumivu makali Manula ambaye alionekana kushika nyonga yake na kulazimika kutoka dakika mbili baadaye na nafasi yake kuchukuliwa na Kawawa.

Kazi nzuri iliyofanywa na Tarryn Allarakhia nusura iipatie Stars bao dakika ya 33, alipomimina krosi safi, lakini kabla haijamkuta Haji Mnoga, iliokolewa kwa

ENDELEA UKURASA 23

# Bosi wa waamuzi aunga mkono VAR, ujio wa marefa kutoka nje

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEKITI wa Kamati ya Waamuzi Nchini, Nassor Hamdoun, ameunga mkono tamko la Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF) kuwa msimu ujao Ligi Kuu Tanzania Bara itatumia teknolojia ya kuwasaidia waamuzi VAR kwa baadhi ya mechi, huku pia akipongeza kuwepo kwa waamuzi kutoka nje ya nchi watakaochezesha baadhi ya mechi.

Hamdoun amesema hayo siku moja tu baada ya Rais wa TFF, Wallace Karia kutamka rasmi kuwa msimu ujao kwa mara ya kwanza, Ligi Kuu itatumia VAR mbili kwa ajili ya kusaidia waamuzi, moja ikiwa ni msaada kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), na nyingine itanunuliwa na mmoja wa wadhamini wa Ligi Kuu waliopewa haki ya kuonyesha michezo ya ligi kwenye televisheni ambao wataleta VAR inayohamishika 'Mobile VAR.'

Hamdoun pia aliunga mkono wazo la kuwatumia waamuzi kutoka nje ya nchi akisema italeta chachu na kuwafanya hata waamuzi wa hapa nchini kuwa makini na uchezeshaji wao.

"Rais karia ametamka wazi kuwa tukijaaliwa msimu ujao tutakuwa na VAR na sisi tunamuunga mkono kwa hilo jambo na tunampongeza kwa niaba ya Kamati ya Waamuzi, tunaomba alisimamie hilo ili kuondoa sintofahamu iliyokuwa inajitokeza viwanjani, sasa marefa wana uwezo wa kurudia kuangalia tukio na kujiridhisha kabla ya kutoa maamuzi sahihi.

"Tutambue kuwa VAR ni moja

ENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >